

**GUARDIOLA ASAINI MIAKA MIWILI MAN CITY**

UKURASA 22

**FUSO** yaparamia watu, yaua wanne na kujeruhi sita

UKURASA 2

**BENKI** Kuu yaonya matumizi ya fedha za kigeni ununuzi wa bidhaa nchini

UKURASA 3

**WABANDIKA** kope watahadharishwa maambukizi ya magonjwa macho

UKURASA 5

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumamosi Novemba 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581869

www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Mbowe na Sugu watiwa mbaroni



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe



Joseph Mbilinyi 'Sugu'



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Augustino Senga

**WADAIWA** kukiuka ratiba ya kampeni, CCM yatoa neno... *Endelea ukurasa wa 2*

## Rais Samia aeleza dunia Tanzania itakavyolisha nchi za Afrika

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizindua kitabu cha ripoti 114 za utafiti wa biashara zilizoandaliwa na watafiti wa masuala ya biashara, wakati akifungua kongamano la tano la Maendeleo ya Biashara na Uchumi, jijini Dodoma jana. Wengine ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Dk. Kennedy Hosea (wa pili kulia), na Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Edda Lwoga. **Habari Uk. 3. PICHA: OWM**

**RIPOTI MAALUM**

# Matumizi akili mnemba bomu jipya watoto chini ya miaka 13

UKURASA 4

**MICHEZO** **SIMBA YAJIIMARISHA KILELENI** UK. 24 **KATUNI** UK. 6

# Ajali Fuso yaua wanne na kujeruhi sita

**Na Vitus Audax**

WATU wanne wamefariki dunia na wengine sita kujeruhiwa baada ya lori aina ya Mitsubishi Fuso lililokuwa limebeba mawe, kuacha njia na kuparamia wananchi na wafanyabiashara katika eneo la Mataa Bunda Mjini, mkoani Mara.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mara, Mrakibu Msaidizi Augustine Magere, alithibitisha jana kutokea kwa ajali hiyo kwa njia ya simu na kusema alipokea taarifa ya tukio hilo majira ya saa 5:40 asubuhi.

Alisema alipokea taarifa hizo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vicent Naano, kuwa kuna ajali katika maeneo ya mzunguko Bunda, eneo la barabara iendayo Ukerewe akimtaka kutuma askari kwa ajili ya shughuli za ukoaji.

"Baada ya kupokea taarifa hiyo na kuwa katika eneo hilo kuna shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo gereji, ambako tulitaarifiwa kuwa gari liliacha njia na kuparamia jengo hilo wakati watu wakiendelea na shughuli zao za kawaida," alisema Magere.

Pia alisema alituma kikosi cha askari 10 kwenda eneo la tukio na kuwa mpaka wakati huo alikuwa hajathibitishiwa juu ya majeruhi na vifo katika tukio hilo.

"Kwa sasa bado hatujawa na taarifa kamili kwani bado shughuli ya uokozi inaendelea, katika jengo hilo lakini taarifa kamili tutazipata baada ya askari wetu kukamilisha shughuli hiyo kukamilika tutaweza kuthibitisha," alisema Magere.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Dk. Steven Wambura, alithibitisha kwamba watu wanne walikuwa wamefariki dunia huku majeruhi wakiwa ni sita ambao bado wanaendelea na matibabu.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Wachuuzi wa mkaa wakisubiri wateja katika eneo la Kivule, jijini Dar es Salaam jana. Bidhaa hiyo, inauzwa kwa bei ya 1,500/- hadi 80,000/-, kulingana na ujazo wake. Licha ya kuwa watu wengi hutumia nishati hiyo kwasababu ni rahisi kupatikana na kumudu gharama zake, tofauti na umeme na gesi, mkaa unatajwa kuwa hatari kwa mazingira. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbowe, Sugu watiwa mbaroni

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Songwe, limemkamata Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, pamoja na vigogo aliokuwa nao kwenye msafara wa kampeni mkoani humo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Augustine Senga, amethibitisha kumshikilia Mbowe na makada wengine 11 wa CHADEMA, kwa madai ya kufanya mkutano wa kampeni eneo ambalo hawakupangiwa.

Katika kundi hilo pia yumo Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo Mkoa wa Songwe, Elia Zambi.

Awali taarifa zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii mapema jana zilidai kuwa Mbowe na wenzake walikamatwa na kupelekwa kwenye mapori, hali ambayo iliibua taharuki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda Senga, alisema viongozi na wafuasi hao walikamatwa katika eneo la Lwati, wilayani Mbozi baada ya kufurushwa eneo la Mlowo, walikokuwa wakilazimisha kufanya mkutano kinyume cha ratiba ya wasimamizi wa uchaguzi.

Alisema mbali na kosa hilo, viongozi hao wanadaiwa kufanya vurugu wakati wa ukamataji na kujeruhi askari wawili.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema jana katika taarifa yake kwa vyombo vya habari kuwa Mbowe alikamatwa baada ya polisi kuvamia msafara wake katika pori la Halungu, lililoko wilayani Mbozi, mkoani humo.

Alisema mkutano wa kwanza ulipangwa kufanyika katika mji wa Mlowo, ulizuiwa na polisi ambao waliwatawanya wananchi kwa mabomu ya machozi. Alisema CHADEMA ilialikwa kwenye mkutano huo ulioandaliwa na ACT-Wazalendo.

"Kabla ya kuwakamata walifuatwa na gari la polisi ambalo lilikutana nao njiani, hivyo liligeuza na baada ya mwendo kidogo walikuta njia imefungwa na magari ya polisi, ndipo walipofungua milango kwa nguvu na kuanza kuwashambulia waliokuwa kwenye magari na kuwakamata kwa nguvu," alisema Mrema.

Alilitaka Jeshi la Polisi liwaachie viongozi hao bila masharti yoyote ili waendelee na ratiba ya mikutano ya kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

"Tunalaani kitendo hiki kwani kinaonesha wazi kuwa ni mkakati wa Polisi, kuhujumu kampeni za chama chetu kwa kushirikiana na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Tunaialika Jumuiya ya Kimataifa, kuja kushuhudia uvunjifu wa haki za kidemokrasia kwa vyama vya upinzani nchini katika uchaguzi huu unaoendelea," alisema Mrema.

Hata hivyo, alisema Mbowe alikamatwa akiwa amefanya mikutano ya kampeni katika Kata ya Itaka, Kijiji cha Itewe na Kata ya Halungu Mjini.

Kwa mujibu wa Mrema, viongozi wengine waliokamatwa ni Mwenyekiti CHADEMA Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi, mbunge mstaafu wa Mbozi Mashariki, Pascal Haonga, Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Wilaya ya Mbozi na Mkuu wa kitengo cha digitali cha CHADEMA, Appolinary Boniface na Mwenyekiti wa chama hicho, Wilaya ya Mbozi, Michael Msongole.

Wengine ni maofisa habari CHADEMA Kanda ya Nyasa, Paul Joseph na Calvin Ndabila, mwanaharakati na kada wa chama hicho, Mdude Nyagali na wasaidizi watatu wa Mbowe ambao ni Adamu Kasekwa (35), Halfan Mbire (37) na Mohammed Ling'wanya, wanaodaiwa kukutwa na visu ambazo ni silaha zisizoruhusiwa kuwepo kwenye mikutano ya kisiasa.

**CHADEMA NYASA**

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Grace Shio, alipinga sababu zilizotolewa na polisi kuhusu kukamatwa kwa viongozi wao, akidai kuwa ukamataji uliofanywa si halali.

Alisema viongozi hao walikamatwa wakiwa wanarejea katika mkutano wa kampeni katika kijiji cha Itewe, hivyo hakuna kiongozi aliyefanya mkutano katika eneo ambalo halikupangwa.

"Wakati viongozi wetu wanarudi wakiwa katika kijiji cha Halungu, walikutana na gari la OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya) ya Mbozi, lakini wakiwa wanaendelea na safari ghafla mbele walikuta magari likiwamo la Halmashauri (limetambuliwa) yakiwa yamefunga njia na kuzuia msafara kisha askari kuanza kuwakamata viongozi wetu," alisema Shio.

Alisema kwa mujibu wa ratiba, chama hicho kilikuwa kifanye mikitano yake katika majimbo mawili mkoani Songwe ambayo ni Mbozi na Tunduma.

"Wametuharibia mikutano yetu mikubwa ya Vwawa na Tunduma, hivyo tunaomba jeshi la polisi liwaachie bila masharti," alisema.

**CCM: TUTAHESHIMU RATIBA**

Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kitaheshimu ratiba zote za kampeni zilizowekwa na kuwaomba viongozi wa watendaji wake, waoneshe hilo katika maeneo yote.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, aliyasema hayo jana katika Kata ya Vingunguti, Jimbo la Segerea, Dar es Salaam, ikiwa ni siku ya tatu tangu kuanza kwa kampeni za Serikali za Mitaa.

Makalla ambaye ni mlezi wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema mbali ya kufanya kampeni za kistaarabu, CCM kama chama kiongozi kitaheshimu ratiba zote za kampeni zilizowekwa.

"Niwaombe viongozi na watendaji muoneshe hilo kwa sababu leo (jana), asubuhi kule Songwe kuna chama fulani sintokitaja, kimekurupuka, kulikuwa na katiba ya Chama cha ACT Wazalendo, lakini wao wanataka kufanya mkutano kukatokea sintofahamu."

"Sisi hatutakuwa kama wale wanaovamia na kushindwa kuheshimu ratiba za kampeni, sisi tutaheshimu," alisisitiza.

Makalla alisema hawatatumia ukubwa wa chama chao kuvunja taratibu na ratiba za kampeni.

Alisema mpaka wanafika hatua hiyo ya kampeni wamepitia michakato mbalimbali na kusisitiza kwamba, ahadi ya CCM ni kufanya kampeni za kistaarabu na kutumia 4R za Rais Samia Suluhu Hassan.

Aidha, aliwaeleza wana CCM kupiga kura ya ndio hata kwenye maeneo ambayo wako.

Alisema CCM ndio chama cha matumaini na kinachoaminika na kuwataka wapinzani waliko wajiunge CCM na kwamba maandamano yaliyofanyika nchi nzima yaliwanufaisha viongozi na si waandamanaji.

"Leo (jana) mwenyekiti kajikakamua na ratiba yake nimeiona na ninawasubiri jukwaani CCM haina utani tumejipanga mitaa yote inakwenda chama tawala," alisema.

Aliwataka mabalozi, kamati za tawi, za kampeni za kata, za siasa wilaya na mkoa wahakikishe wenyeviti wa CCM ndio washinda.

**Imeandikwa na Restuta James na Romana Mallya (Dar), Moses Ng'wat, Songwe.**

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

# Samia aeleza dunia Tanzania itakavyolisha Afrika

**Na Joseph Mwendapole**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema katika mkutano wa nchi zenye uchumi mkubwa duniani (G20) alipata nafasi ya kueleza mikakati ya Tanzania ya kujitosheleza kwa chakula na kulisha nchi zingine za Afrika.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano huo wa G20 uliofanyika Rio De Janeiro, Brazil Jumatatu na Jumanne wiki hii.

Rais Samia alisema kama Tanzania haitakumbwa na madhara makubwa ya mabadiliko ya tabianchi, itakuwa na uwezo wa kujitosheleza kwa chakula chake na kulisha majirani.

Alisema pamoja na hayo bado kuna maeneo ambayo iwapo yataongezewa nguvu, hali ya uzalishaji wa chakula itakuwa bora zaidi na kutaja mambo hayo kuwa ni utafiti mbalimbali, matumizi ya mashine na mbolea.

Kwa mujibu wa Rais, bado dunia inakabiliwa na tatizo la njaa na nchi nyingi zimeweka mikakati ya kupunguza njaa na nchi zilizoendelea zimeahidi kutoa msaada wa kifedha na kiufundi kuondoa njaa.

"Tanzania tulipopewa nafasi ya kuzungumza tulisema kama hatutapata shida ya mabadiliko ya tabia nchi tutakuwa na uwezo wa kuzalisha ziada na kuwauzia wenzetu wa mataifa mengine jirani.

"Tuna vikwazo ambavyo tukisaidiwa kuondokana navyo tutakwenda kwa kasi zaidi katika kilimo, mfano masuala ya kutumia zana za kisasa katika kilimo kama mashine za kuvunia na kumwagilia. tukipata hayo na kwa ardhi tuliyo nayo tutakwenda kwa kasi kubwa sana," alisema.

Tatizo lingine, alisema ni uhaba wa mbolea hali ambayo inasababisha kuagiza nje ya nchi na kwamba kazi kubwa iliyopo ni kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya mbolea ili kujitosheleza na kuachana na utegemezi.

"Tukiweza kutumia mbolea sahihi na tukawa na mbolea inayojitosheleza tutalisha wenzetu wa Afrika kwasababu kama leo hii tunauza baadhi ya bidhaa hadi China inamaanisha tukijipanga vizuri tunaweza kabisa kufanya vizuri," alisema. Kuhusu nishati safi, alisema lengo la viongozi wa Afrika ni kwamba ifikapo mwaka 2030 watu milioni 300 wawe wameshapata umeme. Alisema hivi sasa watu milioni 700 Afrika hawana umeme kabisa hivyo wamejiwekea malengo angalau ikifika mwaka 2030 watu milioni 300 wawe wameshapata umeme.

"Sasa (mwaka) 2030 tukijaliwa na mambo yakaenda vizuri namimi nitakuwa nimemaliza dhamana hii niliyopewa kwa hiyo nitajidai kuwa nimewezesha watu hao kupata umeme," alisema.

Rais Samia alisema kando ya mkutano wa G20 alipata nafasi ya kukutana na viongozi wa nchi mbalimbali na wakuu wa taasisi za kimataifa ambapo walijadili ushirikiano uliopo, miradi na maeneo mapya ya uwekezaji.

Alitaja baadhi ya viongozi aliokutana nao kuwa ni Waziri Mkuu wa Norway ambaye walijadili kuhusu ajenda ya nishati safi ya kupikia, Rais wa Misri ambaye walijadili mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere JNHPP na Waziri Mkuu wa Vietnam waliyejadiliana kuhusu ushirikiano katika sekta ya mawasiliano.

Pia alisema alikutana na Rais wa Indonesia, ambaye walijadiliana kuhusu ushirikiano uliopo kwenye sekta ya mafuta na gesina marais wa benki ya dunia na benki ya maendeleo Afrika.




Waendesha bodaboda, wanafunzi na wadau mbalimbali, wakiwa kwenye maandamano ya kampeni ya kupinga vita dhidi ya rushwa ya ngono, eneo la Mbagala Dar es Salaam juzi. Kampeni hiyo inasimamiwa na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), kwa ufadhili wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (Women Fund Tanzania Trust). **PICHA: SABATO KASIKA**

# BoT yaonya matumizi ya fedha za kigeni ununuzi bidhaa nchini




**Na Jenifer Gilla**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imeonya kuhusu matumizi ya fedha za kigeni nchini kwenye mauzo ya bidhaa au huduma kuwa ni kinyume cha Sheria ya Benki Kuu Kifungu cha 26. Onyo hilo limetolewa wakati ikishuhudiwa baadhi ya wauza bidhaa na watoa huduma kutaka kulipwa kwa fedha za kigeni hasa dola hali inayoleta usumbufu kwa wateja. Taarifa iliyotolewa juzi na benki hiyo kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram imeeleza kuwa imebaini uwapo wa baadhi ya bidhaa na huduma kuendelea kufanyika kwa kutumia fedha za kigeni, jambo ambalo ni kinyume na sheria ya benki hiyo. "Bidhaa na huduma hizo ni pamoja na kuuza au kupangisha nyumba, viwanja na ofisi, ada za shule, pamoja na malipo na ushauri," ilieleza taarifa hiyo. Aidha, taarifa hiyo imewahimiza wananchi kutoa taarifa kwa benki hiyo pale wanapolazimishwa kulipia huduma kwa kupitia fedha za kigeni ili sheria ichukue mkondo wake.

Kadhalika iliwakumbusha wananchi kuwa ni muhimu kutumia Shilingi ya Tanzania wakati bei na kufanya malipo ya bidhaa na huduma ili kuendelea kuimarisha uchumi.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya BoT, matumizi ya shilingi nchini yataiwezesha benki hiyo kutekeleza sera ya fedha ili kuwezesha kuwapo kwa utulivu wa bei za bidhaa na huduma nchini. Pia ilisema kupunguza matumizi ya fedha za kigeni yasiyo ya lazima ili kuimarisha thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni. "Matumizi ya shilingi nchini yataimarisha ustahamilivu wa sekta ya fedha na kuvutia wawekezaji hivyo kuongeza pato la nchi na kuinua uchumi kwa ujumla," ilisema taarifa hiyo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Majaliwa: Andaeni Mitaala kuwezesha vijana wetu kujiajiri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amevitaka vyuo vya biashara nchini kufanya mapitio ya mitaala ili kuwajenga wasomi wenye uwezo wa kutumia elimu zao kujiajiri, badala ya kuendelea kusubiri nafasi chache za ajira serikalini.

Majaliwa alisema hayo jana jijini hapa kwenye kongamano la kitaaluma la kuwasilisha matokeo ya utafiti kuhusu biashara na mazingira wezeshi kwa maendeleo jumuishi, lililoandaliwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

"Vyuo vya biashara fanyeni mapitio ya mitaala yenu ili tuwe na mitaala inayojenga wasomi wetu kupenda kubuni na kufanya biashara, wasomi wetu wa sekta ya biashara zingatieni mtaala wa biashara ili kila msomi anapomaliza masomo afikirie zaidi kufanya biashara kuliko kusubiri kuajiriwa serikalini.

"Serikalini nafasi zenyewe zimejaa na wengi ni vijana wana miaka 30, kwa hiyo ili mwingine atoke hapo mpaka awe na miaka 60. Kuna miaka mingine 30 ya kusubiri hivyo wahitimu wakiendelea kusubiri ajira serikalini wataendelea kuilaumu serikali kila siku," alisema Majaliwa.

Aidha, alisema ili kumaliza tatizo hilo, vyuo vya biashara vipitie mitaala yake na kuanza kuwajenga wasomi baada ya kuhitimu masomo yao watumie elimu yao kufanya yale waliyosoma kubuni miradi itakayowaingizia kipato.

"Nilipokwenda kufanya ziara Kilombero nilikutana na vijana wawili wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA), ambao wameamua kufanya biashara ya mchele na masoko yao wanayapata kwenye shule za bweni na maeneo mengine, hivyo natamani vijana wengi wahitimu wa vyuo wawe na mawazo kama hayo ya kujiajiri badala ya kusubiri ajira za serikali," alisema.

Vile vile, aliiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara, kushirikiana na taasisi za umma na binafsi, kufikiria namna ya kuongeza ujasiriamali nchini kwa rika zote.

"Nihimize wataalam wetu kwenye taasisi za elimu kufanya tafiti na mtumie matokeo ya tafiti zenu kuboresha mazingira ya biashara, ikiwemo utengenezaji wa bidhaa hii itasaidia sana kuongeza tafiti na bidhaa zetu kuingia kwenye ushindani," alisema.

Kadhalika, Majaliwa aliiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine, kuimarisha mifumo ya biashara kuanzia ngazi ya shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati pamoja na vyuo vya elimu ya juu, ili ikidhi mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya kiuchumi na teknolojia.

Mkuu wa huo cha CBE, Prof. Edda Lwoga, alisema kongamnao hilo ni la tano kufanyika tangu mwaka 2019 ambapo jumla ya matokeo ya tafiti 114 yatawasilishwa.

Alisema lengo la kungamano hilo ni kujadiliana na kubadilisha uzoefu kuhusu tafiti zilizofanyika, zenye lengo la kuangalia fursa za kibiashara zilizopo na changamoto zake ili kuzitafutia ufumbuzi.

# Matumizi akili mnemba bomu jipya watoto chini ya miaka 13

Na Jenifer Gilla

LICHA ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuelekeza kuwa matumizi ya akili mnemba yaanzie kwa watoto wa miaka 13, nchini Tanzania hali ni tofauti kwa wanafunzi chini ya umri huo.

Septemba 7, 2023 UNESCO ilitoa mwongozo wenye vipengele saba unaotaka nchi kudhibiti matumizi ya akili mnemba mashuleni ikiwamo kuwa na sera ya matumizi kimaadili katika elimu na utafiti.

Mwongozo huo unataka kuwe na faragha na umri wa matumizi uanzie miaka 13 pamoja na kuwapatia walimu mafunzo kuhusu teknolojia hiyo.

Nchini Tanzania, baada ya kubainika changamoto ya watoto chini ya umri huo kutumia akili mnemba kujibu maswali wanayopewa na walimu shuleni, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika mahojiano maalum na Nipashe imesema hivi karibuni itatoa mwongozo.

**HALI ILIVYO SASA**

Baadhi ya wazazi wenye watoto wanaosoma shule za msingi za binafsi ambao wapo chini ya miaka 13, wamekiri watoto wao kutumia akili mnemba kujibu maswali wanayopewa na walimu ili kufanyia nyumbani, yaani 'homework'. Wanasema changamoto hiyo inasababishwa na baadhi ya maswali wanayopewa watoto wao kuwa magumu kwao kama wazazi.

Wanasema huwapa vifaa vya kieletroniki kama simu au kompyuta na mifumo wanayotumia zaidi ni Chat GTP au gemini ili kuwarahisishia kutafuta majibu ya maswali wanayopewa na walimu.

Mkazi wa Goba, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Ester Japhet, mwenye mtoto anayesoma darasa la tano, anasema amelazimika kumfundisha mtoto wake kutumia Chat GTP kujibu maswali anayopewa na walimu shuleni kwa sababu mengi hayamo kitabuni.

"Alianza kutumia Chat GTP tangu mwaka jana wakati huo akiwa darasa la nne, kwa sasa yupo darasa la tano, binafsi ninaona ni njia rahisi kwake na mimi nina majukumu mengi.

"Unajua kuna baadhi ya maswali mtoto anakuja nayo nyumbani hata wewe mzazi hujui jibu inabidi uhangaike mitandaoni kutafuta majibu. Au kuuliza watu mbalimbali kutafuta majibu, njia ambayo unajikuta unapoteza muda mwingi. Tangu nilipomfundisha Chat GTP hivi sasa anajitegemea," anasema.

James Macha, mkazi wa Tabata, Dar es Salaam, mwenye mtoto wa darasa la sita, anaungana na mzazi aliyetangulia kwamba, mtoto wake anatumia mfumo huo baada ya bosi wake kumwelekeza namna ya kuutumia ili kumsaidia mwanaye.

Anasema kutokana na elimu yake kuwa ya kawaida, amekuwa akishindwa kumsaidia mtoto wake na kulazimika kuomba msaada kwa watu mbalimbali. Anasema alimwelekeza mtoto wake matumizi yake na sasa anaitumia kufanya maswali ya darasani.

Kuhusu ufaulu wa mtoto wake, Macha anasema ni wa kawaida na mara nyingi hushika nafasi ya 20 kuendelea kati ya watoto 32 darasani kwao.

Mzazi mwingine, Mwanaisha Saidi, anatofautiana na wenzake anasema, aliacha kumpa mtoto wake akili mnemba baada ya kuona ameanza kuwa tegemezi hata kwa maswali ya kawaida.

Anafafanua kuwa hata alipopewa swali ambalo analifahamu alikuwa akimwomba amwekee Chat GDP ili atafute jibu. Anasema aligundua katika kipindi cha miezi mitatu cha mtoto wake kutumia mfumo huo, ufaulu wake darasani ulishuka na katika mitihani yake aligundua alikosa baadhi ya maswali ambayo yapo ndani ya uwezo wake.

"Nilizungumza na mwalimu wake wa darasa nikamweleza kuwa huwa nampa Chat GDP kutafuta majibu kwa sababu mimi ratiba yangu ni ngumu, kazi na masomo pia, akaniambia mfumo huo si mzuri unalemaza watoto hivyo niache mara moja," anasema.

**KAULI ZA WALIMU**

Mwalimu wa Shule ya Msingi Sisters of St Joseph, Dege, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, Justine Kivuyo, anasema mwanafunzi anayetumia Chat GTP hawezi kujengeka vizuri kitaaluma kwa sababu anayefanya kazi hiyo sio yeye.

Anasema lengo la kuwapa wanafunzi kazi za nyumbani ni kuwapunguzia muda wa kufanya mambo yasiyohusiana na taaluma yao kama vile kuangalia luninga kwa muda mrefu, badala yake wakae na wazazi wajadili masuala ya shule ili kukuza taaluma zao.

"Tunapompa mtoto maswali tunataka asumbue ubongo wake hata kama lile swali atakosa. Baadhi ya wazazi wanaamini katika kupata swali ndio maana wanaingia kwenye kutumia Chat GTP ili mtoto apate bila kujua kuwa wanamlemaza," anasema.

Mwalimu wa Darasa la tano katika shule moja ya binafsi jijini Dar es Salaam, Mary Fwaisa, anasema mtoto anapoanzisha matumizi ya mashine katika kutafuta majibu uwezo wake wa kufikiri huwa mdogo na hujifunza kuwa tegemezi.

Anatahadharisha kuwa kwamba kitendo hicho hakiwezi kumsaidia mwanafunzi kitaalum na hivyo, wazazi wanapaswa kuwa kipaumbele kukemea hilo.



Prof. Ladslaus Mnyone

Fwaisa anasema kitaaluma tabia hiyo inarudisha nyuma maendeleo ya ukuaji wa sekta ya elimu na kwamba, jambo hilo lisipotafutiwa ufumbuzi litaleta shida baadaye.

"Kwa mfano, shule zinafungwa mtoto atapewa maswali ya kufanyia nyumbani, kama hatafanya kwa akili yake akatumia huo mfumo kujibu maswali, mwanafunzi anakuwa hajaingiza chochote," anasema.

Anashauri wazazi wanapofanya mikutano na walimu wapewe elimu kuhusiana na madhara ya kutumia mfumo huo kwa watoto wao na kuwa mabalozi wa kuzuia mifumo hiyo.

Mwalimu mwingine kutoka Shule ya Msingi Mgowelo, iliyoko mkoani Iringa, Victor Kalinga, anasema: "Sisi tunataka mzazi awe sehemu ya safari ya kitaaluma ya mtoto wake."

Anasema lengo ni kama kuna sehemu mtoto anarudi nyuma kimasomo na walimu hawajui, mzazi asaidie kutambua na kuwasiliana nao ili kwa pamoja wamsaidie. "Mzazi anapokimbia wajibu huo na kuipa jukumu mashine si salama kwa makuzi ya mtoto" anasema mwalimu Kalinga na kushauri wazazi wawe watu wa kwanza kuzuia watoto chini ya umri tajwa kutumia mifumo hiyo.

Mwalimu wa Taaluma Shule ya Msingi Uhominyi iliyoko Wilayani Kilolo, mkoani Iringa, Silvester Mbata, anasema katika mazingira ya kawaida matumizi ya akili mnemba katika masuala ya kitaaluma hayaongezi chochote.

Anabainisha kuwa humfanya mtoto kushindwa kutumia milango yake ya fahamu kutafakari na kuyatawala mazingira.

"Kwa watoto wadogo ni mbaya zaidi kwa sababu inamwharibu kisaikolojia labda angetumia wakati amekua na anajitambua" anasema na kuonya kuwa hali ikiendelea hivyo kutakuwa na watoto na wataalam hapo baadaye wenye uwezo mdogo katika fani mbalimbali.

**WANASAIKOLOJIA**

Mwanasaikolojiatiba Dk. Saldeen Kimangale anaonesha kuwapo kwa madhara makubwa.

Anasema pamoja na faida zinazopatikana kutokana na matumizi ya teknolojia hiyo, kuitegemea pekee bila ufahamu na kujifunza kuna madhara makubwa kwa watoto ambao wanawajibika kukuza maarifa na ujuzi wao. Anasema moja ya sababu za kutafuta elimu ni kujiweka huru kutokana na utumwa wa ujinga.

Anafafanua kwamba elimu inampa mtu zana za kuyakabili mazingira yake, kupambana na changamoto za maisha na hatimaye kuishi maisha yenyewe, jambo ambalo mtoto hawezi kulipata kwenye akili mnemba.

"Mtoto anayetegemea Chat GPT bila shaka atadumaa katika kujifunza na hasa kufikiri kimantiki na kujenga hoja. Stadi ambazo ni muhimu sana kwa ulimwengu wa sasa na ujao, Chat GPT inakupa majibu kwa mujibu utakachouliza au kutaka kujua, lakini haina uwezo wa kupambanua," anafafanua.

**WADAU ELIMU**

Mkurugenzi wa Miradi na Ushirikiano wa Shirika la CAMFED, Anna Sawaki, analiambia Nipashe kuna haja ya kuandaa miongozo kama UNICEF ilivyoeleza ili kudhibiti matumizi ya teknolojia hiyo kwa watoto.

Anasema kama watoto watapewa uhuru wa kuitumia bila kufuata taratibu za kitaalam, inaweza kuleta madhara makubwa ikiwamo kuwajengea hali ya utegemezi na kuangalia maudhui yasiyowahusu.

Mkuu wa Idara ya Teknolojia ya Habari katika Taasisi ya Jenga Huh, Maron Kakoti, anashauri walimu wanaofundisha watoto wapewe elimu kuhusu matumizi ya akili mnemba, ili wajue ni kwa namna gani watadhibiti au watatumia kujenga uwezo wa wanafunzi.

Anasema si sahihi watoto wa chini ya miaka 13 kutumia akili mnemba kwa sababu akili zao bado hazina uwezo wa kuchuja.

**HAKUNA SHERIA**

Wakili wa Kujitegemea kutoka Kampuni ya Accuracy iliyoko Kinondoni, Dar es Salaam, Bashiru Yakubu, anasema hakuna kanuni, sheria wala miongozo kuhusiana na kazi za kufanya nyumbani wana matumizi ya akili mnemba kwa watoto nchini.

Anasema hata kanuni za Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) kwa mitihani inayofahamika kitaifa zinasema, mwanafunzi anatakiwa afanye mwenyewe mtihani bila usaidizi wowote.

"Hili jambo halina kanuni rasmi na sheria elekezi, inatakiwa waratibu walisimamie katika ngazi zote kwa kuongea na wanafunzi pamoja na wazazi," anasema.

**KINACHOENDELEA SERIKALINI**

Mkurugenzi Idara ya Sayansi na Teknolojia na Ubunifu kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Ladslaus Mnyone, anakiri kuwapo kwa tabia hiyo kwa baadhi ya wazazi.

Hata hivyo, kiongozi huyo anasema Wizara inaandaa mwongozo wa kusimamia matumizi ya akili mnemba kwa wanafunzi ambao utatolewa hivi karibuni.

"Kwa hali ya kawaida mwongozo pekee unaweza usitoshe kwa sasa, kinachotakiwa zaidi ni kuhakikisha tunawafundisha walimu wetu waweze kuwadhibiti vizuri wanafunzi katika matumizi ya teknolojia pamoja na kutoa aina ya maswali ambayo itakuwa rahisi kumbaini mwanafunzi ambaye hajatumia akili yake," anasema.

Prof. Mnyone anasema akili mnemba ni nzuri na italeta tija kwa wanafunzi kama wataitumia vizuri, akisisitiza kuwa katika mwongozo utakaozinduliwa utazingatia maoni ya wadau.

"Maoni hayo yatajikita zaidi katika kuonesha wajibu wa mzazi, walimu na wadau wa elimu uwe vipi, lengo ni kuhakikisha tunatoka na mwongozo utakaokuwa suluhu ya suala hilo," anasema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Wabandika kope watahadharishwa magonjwa macho

**Na Christina Mwakangale**

BINGWA wa Magonjwa ya Macho kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Dk. Yusta Mtogo, ametahadharisha wanawake hasa mabinti, wanaopendelea kuweka kope bandia kwenye macho ili kuboresha mwonekano.

Amesema zipo athari za uwekaji wa urembo huo bandia, kama vile macho kuwa na mzio (allergy), kupata maambukizi, kuwa makavu, mekundu na hata kusababisha kope za asili kutoka machoni.

Bingwa huyo aliyasema hayo jana, Dar es Salaam akisisitiza kwamba ni vyema wanaoweka wakafanya hivyo kupitia watu wenye ujuzi huo, ili kuondoa athari hizo ambazo hasa husababishwa na gundi inayotumika pamoja na kope bandia.

"Kama unapendelea kubandika kope za bandia katika macho unapaswa kuwa makini zaidi, ili kulinda macho yako. Yapo madhara kwa aina ya urembo huo na hata kupata maambukizi ya bakteria.

"Macho huweza kupata maambukizi na kuhisi kama macho yana mchanga, kwa sababu ya kuweka kope kwa muda mrefu au mara kwa mara," alisema bingwa huyo.

Alisema urembo huo huweza kusababisha macho kuwa na matongotongo, hata kuhatarisha kioo cha jicho na kikipata mikwaruzo itasababisha vidonda na makovu kwenye jicho.

"Athari za kope bandia pia mtu anaweza kupoteza kope za asili ambazo kazi yake ni kulinda jicho dhidi ya vumbi, jasho.

"Kope za asili zikitoka husababisha ukavu wa macho na hayo yote akipata mtu ni tatizo afike hospitali kwa ajili ya uchunguzi, matibabu kliniki ya MNH-Mloganzila," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Dk. Mwinyi aanika mikakati ukuaji uchumi

**Na Mwandishi Wetu**




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akihutubia katika hafla ya Utiaji wa Saini wa Mpango wa Maboresho ya Utoaji wa Huduma Bandari ya Zanzibar (Zanzibar Port Improvement), katika viwanja vya Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amebainisha mikakati ya serikali kuhusu ukuaji uchumi wa Zanzibar na kueleza kuwa inaendelea kuwawekea mazingira rafiki wafanyabiashara wote wanaotumia bandari ya Zanzibar.

Dk. Mwinyi amesema hayo jana alipozindua, kutia saini na kushuhudia utiaji wa saini Mpango wa Maboresho ya Utoaji Huduma kwa Bandari ya Zanzibar (Zanzibar Port Improvement Charter).

Utoaji huo wa huduma ni kwa ushirikiano wa serikali, wadau wa bandari kutoka taasisi za umma na binafsi pamoja na Taasisi ya Tony Blair (TBI).

Alisema lengo la mpango huo ni kuondosha usumbufu kwa kupeana majukumu kwa kila mdau, kupitia viashiria vilivyoandaliwa ndani ya mpango huo sambamba na kurahisisha ushushaji wa makontena (makasha).

Pia ukaaji wa meli ukutani, kusubiria ukuta pamoja na masuala ya 'Customes Clearance' kwa kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za bandari ili kutoa msukumo wa ukuaji wa uchumi wa nchi. Kuhusu upakiaji na ushushaji wa makontena bandarini, Rais Mwinyi amewahakikishia wafanyabiasha wa Zanzibar kwamba, serikali imedhamiria kwa dhati kuimarisha utoaji wa huduma kwa kurahisisha mchakato huo katika bandari zote nchini.

Alisema hatua hiyo ni kwa mujibu wa wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 hadi 2025 katika Ibara ya 167(b) inayozungumzia kuimarisha huduma za bandari kwa kutumia vifaa na teknolojia za kisasa.

Lengo la kufanya hivyo, alisema ni kuongeza idadi ya makontena kutoka 82,312 mwaka 2018 hadi 105,000 ifikapo 2025 na kupunguza siku za kuegesha meli kutoka siku saba mwaka 2018 hadi siku tano mwaka 2025.

Alisema kwa sasa uwezo wa bandari za makasha tatu; Malindi, Fumba na mkoani Pemba zina uwezo wa kuhudumia makasha zaidi ya 105,000.

Rais Mwinyi alisema makubaliano hayo baina ya serikali na taasisi hizo ni utekelezaji na ufanisi kwa Bandari ya Zanzibar pia, kutafanyika upimaji wa kila kilichotekelezwa na taasisi hizo kila inapotimia mwaka mmoja.

Alisema endapo taasisi zote zitatekeleza wajibu wao ipasavyo, mafanikio makubwa yatapatikana nchini, akitolea mfano nchi za Singapore, Mombasa-Kenya, Gambia kwa kufanikiwa na mpango kama huo wa utoaji huduma wa bandari ambao wamepiga hatua kubwa ya mafanikio.

Katika hatua nyingine ya kuboresha huduma za bandari Rais Mwinyi alisema, serikali inatarajia kuanza ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani inayotarajiwa kuhudumia meli kubwa za mafuta na gesi.

Alisema ujenzi wa bandari hiyo unakwenda sambasamba na Ilani ya Chama cha Mapinduzi CCM, kifungu 167(c) kinachoielekeza serikali kujenga miundombinu ya kuhudumia meli zinazopita mwambao wa Afrika Mashariki, kupata huduma za kuongeza mafuta, maji safi na kufanya matengenezo.

Rais Mwinyi aliwataka wadau wa bandari ya Zanzibar ikiwamo Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi yenye kubeba jukumu kubwa la taifa la kusimamia miundombinu nchini.

Kadhalika alisema kuendelea kuwa karibu na watumiaji wa miundombinu hiyo kwa kuwapelekea huduma na nyenzo ili kuhakikisha wananchi wanatumia miundombinu bora na yenye tija kwa ustawi wa jamii na kuinua uchumi wa Zanzibar kwa maendeleo ya wananchi.

Rais Mwinyi alisema jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi wanashirikiana na wadau mbalimbali kuendeleza sekta ya Uchukuzi.

Aliwaomba wafanyabiashara waendelee kufanya kazi zao kwa uaminifu, maadili na uzalendo ili kujipatia kipato halali na kuzingatia wajibu wao wa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Dk. Khalid Salum Mohamed alisema kusainiwa kwa mpango huo ni makubaliano baina ya serikali na wadau wa bandari hiyo zikiwamo taasisi za umma na binafsi kufanyakazi kwa pamoja ili kuongeza ufanisi na kuleta tija katika kukuza Uchumi wa nchi.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari, Akif Ali Khamis alipongeza hatua ya serikali kuleta mapinduzi makubwa kwa sekta ya bandari ya Zanzibar kuhusu uendeshaji wa bandari hiyo baada ya kuingia mkataba na Kampuni za Zanzibar Multiple, kampuni ya Bandari ya Fumba na ya Mkoani kwaajili ya kushusia makasha (makontena.

Kiongozi wa timu ya Taasisi ya Tony Blair, Frank Matsaert alisifu juhudi za serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuusimamia hadi kuufanikisha mpango huo na kueleza kwamba utakwenda kufungua mafanikio ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kupitia lango la Bandari hiyo.

# Uhalifu mtandaoni waundiwa kikosi kazi

**Na Grace Mwakalinga**

SERIKALI imeunda kikosi kazi maalumu kitakachokuwa chini ya Wizara nne za kisekta kushughulikia matukio ya uhalifu mtandaoni huku kipaumbele kikiwa ni kwa mikoa inayoongoza kwa matukio hayo.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi , Hamad Yussuf Masauni, alisema hayo hiyo jana wakati wa kikao cha majumuisho kilichohusisha Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kampuni za simu.

Alitaja wizara zitakazoshughulikia matukio hayo kuwa ni Katiba na Sheria; Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; na Mambo ya Ndani ya Nchi.

Alisema hatua hiyo imetokana na kukithiri kwa matukio ya uhalifu wa mtandaoni, akitaja mikoa ya Rukwa, Mbeya, Morogoro na Dar es Salaam.

Waziri alisema makatibu wakuu wa taasisi hizo watakutana kujadili ni kwa namna gani watatekeleza mkakati wa kukabiliana na matukio ya uhalifu na baadaye mawaziri watakutana.

"Tumeunda kikosi kazi hiki ili kuongeza nguvu kukabiliana na vita dhidi ya uhalifu wa mtandaoni, vitendo hivyo vimeleta madhara makubwa kwa wananchi, ikiwemo kuibiwa mali na fedha zao," alisema Masauni.

Waziri Masauni alisema umuhimu wa kuwekeza rasilimali watu na vifaa katika kukabiliana na uhalifu wa mtandao, umeleta tija baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hasaan, kuongeza bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani (ya Nchi) ili kukabiliana nao. Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, alisema matumizi ya teknolojia kama vile akili mnemba (AI), yamerahisisha utendaji kazi katika kupambana na uhalifu wa mtandao.

Alisema hadi kufikia Septemba mwaka huu, laini milioni 80.7 za mitandao ya simu zilikuwa zimesajiliwa.

Alitoa rai kwa wananchi, taasisi za serikali kama Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na kampuni za simu, kuendelea kuwaelimisha wananchi, huku akiwataka watumiaji wa huduma za mawasiliano kutotoa namba za siri na kutoa taarifa kwa jeshi la polisi kuhusu wizi wa laini ili kusaidia uchunguzi na mashtaka kufunguliwa.

Aidha, aliitaka BoT kuongeza usimamizi wa mawakala na kuongeza masharti ya kusajili taasisi zinazojihusisha na fedha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF msipuuzie taarifa za wadau mitandaoni

**WIKI** hii imekuwa wiki ya furaha kwa wapenda soka na watanzania kwa ujumla baada ya kushuhudia timu ya soka ya taifa 'Taifa Stars' kufuzu fainali za Afrika zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Taifa Stars imefuzu baada ya kupata ushindi muhimu kwenye mchezo dhidi ya Guinea ambao Stars walikuwa wakihitaji zaidi ushindi ili kujihakikishia nafasi ya kushiriki fainali hizo zitakazofanyika mwezi Desemba, 2025.

Mchezo huo ulivuta hisia za mashabiki wa soka wa Tanzania, Guinea na maeneo mengine ya Afrika kutokana na ukweli kuwa ndio mchezo uliokuwa ukitoa timu ya pili itakayoungana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kutoka kwenye kundi lao kufuzu kwa fainali hizo.

Hata hivyo, siku chache baada ya Stars kujihakikishia tiketi ya kushriki fainali hizo, zimeibuka taarifa kwenye mitandao ya kijamii zikielezea uwezekano wa Tanzania kupokonywa pointi tatu kutokana na kumchezesha mchezaji (Muhamed Ame) akiwa amevaa jezi yenye namba ambayo haikuorodheshwa kwenye fomu ya wachezaji wa mchezo huo.

Katika fomu hiyo jina la Ame lilikuwepo lakini ilionyesha angevaa jezi namba 24 na si 26 ambayo alikuwa amevaa siku hiyo na kuingia uwanjani dakika ya 76 ya mchezo.

Siku chache baada ya mchezo huo huku watanzania wakiwa bado kwenye shangwe za kufuzu, mwanamitandao mmoja wa nje ya nchi aliandika uwezekano wa Tanzania kupokonywa pointi tatu kwa kosa hilo huku akiainisha baadhi ya vifungu vya kanuni za CAF.

Bila kificho taarifa hiyo ilianza kuleta taharuki kwa mashabiki wa soka nchini ambao walianza kuingiwa hofu ya kupokonywa nafasi ya kushiriki fainali hizo kwa mara ya nne.

Licha ya Shirikisho la soka Tanzania haraka kutoa ufafanuzi na kuwatoa hofu mashabiki juu ya taarifa hizo, bado TFF inapaswa kutoa taarifa ya kina kuweka mambo sawa kwa mashabiki.

Taarifa waliyoitia juzi kupitia Afisa habari wake, Clifford Ndimbo mashabiki wengi wanaona haijajitosheleza kulinganisha na taarifa ya mwanamitandao huyo aliyoitoa.

TFF isipuuzie uvumi uliopo na badala yake kama chombo cha kusimamia mpira kitoe ufafanuzi wa kina ikiwezekana na wao kuainisha vifungu vya kanuni ili kuondoa hofu mashabiki wa soka na watanzania kwa ujumla.

Na ikiwezekana Nipashe tunashauri TFF kupitia kitengo chake cha habari chini ya Ndimbo kiitishe mkutano na waandishi wa habari kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kwa watanzania.

Kwa sasa kutokana na maendeleo ya teknolojia, dunia ipo kiganjani na taarifa yoyote ni rahisi kusambaa kwa haraka kutokana na uwepo wa mitandao ya kijamii, kitu ambacho kama taarifa si ya kweli au ni ya kweli inaleta taharuki kwa haraka zaidi.

Kwa sasa wapo walioielewa taarifa ya ufafanuzi ya TFF, lakini pia wapo ambao hawajailewa wakilinganisha na taarifa iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii ya wasiwasi wa kupokonywa ushindi kwenye mchezo dhidi ya Guinea.

Licha ya yote tunaipongeza timu yetu ya taifa 'Taifa Stars' kwa kuweza kufuzu fainali hizo za mwakani zaitakazofanyika nchini Morocco kuanzia mwezi Desemba , 2025.

Lakini pia pongezi ziende kwa Serikali kwa kuiunga mkono timu ya taifa pamoja na Shirikisho la soka Tanzania kwa usimamizi wao mzuri wa kanuni, taratibu na sheria zote za soka.

Ushindi walioupata Stars si wa wachezaji na viongozi wa soka peke yao, bali na wa watanzania wote bila kujali itikadi za dini, vyama vya siasa wala ushabiki wa soka, ni timu ya watanzania wote, ni ushindi wa watanzania wote, Tanzania imefuzu kwa mara ya nne fainali za AFCON.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Che Malone sasa anastahili kupewa unahodha Simba

**KUNA** tabia ambayo imejengeka kwa timu za Tanzania kuwa nahodha ni lazima awe mzawa.

Sio sheria wala kanuni, ni kama utamaduni tu ambao upo katika klabu za hapa nyumbani.

Hakuna anayekataa anayestahili kuwa nahodha wa timu apewe kitambaa, lakini isiwe kuwa ni lazima awe Mtanzania.

Mfano kabla ya kifo cha kiungo raia wa Rwanda, Patrick Mafisango, alipewa unahodha baada ya kuonekana ni kiunganisho kikubwa baina ya waamuzi na wachezaji wa Simba katika mashindano ya kimataifa.

Awali, Mafisango hakuwa nahodha, lakini katika michuano ya kimataifa walikuwa wanapenda kuzungumza naye ili kupeleka meseji kwa wachezaji wa timu hiyo wakati wa mchezo.

Akaonekana kama yeye ndiye nahodha wa mchezo karibuni kila mchezo wa kimataifa. Labda ilitokana na kufahamu lugha nyingi, kiswahili, kiingereza, kifaransa na kilingala.

Viongozi wa Simba waliliona hilo, wakaamua kumpa unahodha Mafisango hasa kwenye michezo ya kimataifa, kabla ya umauti kumfika hapo mwaka, 2012 kwa ajali ya gari jijini, Dar es Salaam.

Hivi karibuni nimeifuatilia Simba pamoja na wachezaji wake, nimeona kuna mchezaji wa nafasi ya ulinzi, Fondoh Che Malone, ambaye huu ni msimu wa pili kwake akikitumikia kikosi hicho.

Msimu huu amekuwa bora zaidi kuliko uliopita, lakini ukisikiliza mahojiano yake na waandishi wa habari pamoja na wachambuzi, wanavyojieleza, wanavyowaelezea wachezaji wenzake, viongozi na klabu kwa ujumla, anaonekana kuwa ni mtu mwenye kaliba ya uongozi.

Hata ndani ya uwanja ukimwangalia amekuwa akiwaelekeza wenzake ni nini cha kufanya na wakati gani, wakati mwingine wakiwafokea wenzake ambao wanafanya 'fyongo' uwanjani.

Binafsi naona kabisa iwapo viongozi wa Simba watazinduka usingizini na kumpa unahodha Che Malone na Mohamed Hussein 'Tshabalala' akabaki kuwa msaidizi inaweza kuwasaidia sana.

Tshabalala siyo nahodha mbaya, lakini kuna wakati amekuwa mpole mno kwa wachezaji wenzake na hata pale anapoona mchezaji wake amefanyiwa faulo kwa makusudi na mwamuzi haonekani kuchukua hatua zozote zinazostahili. Inawezekana labda nje au kambini ni mzuri kwa kuwaunganisha wenzake, lakini linapokuja suala la ndani ya uwanja bado anaonekana ni mpole sana kiasi cha kuifanya wakati mwingine Simba kukosa haki fulani ambazo hupatikana kwa manahodha wanaopenda kwenda kwa waamuzi na kuongea nao mara kwa mara.

Nakumbuka hata mchezo dhidi ya Orlando Pitares ya Afrika Kusini, Simba ilipotolewa kwa penalti michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, bao lile lilikuwa ni lakuotea, lakini hakukuwa na presha ya nahodha kwenda kwa mwamuzi kumtaka akaangalie VAR, ingawa wapinzani walikuwa mstari wa mbele kumshinikiza ili Chris Mugalu aonyeshwe kadi nyekundu na ikawa hivyo.

Kwa muda mrefu nilikuwa sijaona ni nani katika wachezaji wa Simba wanaoweza kuwa manahodha, lakini kwa sasa Che Malone ana sifa zote.

Ukiacha kuwa msemaji na mtetezi wa wachezaji ndani ya uwanja, amekuwa akiongea vitu ambavyo vimekuwa 'vikitrendi' sana kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kutokana na uwezo wake wa kujieleza, kutahmini michezo, kuielezea klabu yake, wachezaji na mengineyo.

Ni tofauti na wachezaji wengi wa Kitanzania ambao ukiwahoji ni kama wamekariri majibu ya mtihani.

"Napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu, tumemaliza mchezo salama, hatuna majeruhi. Tumepoteza mechi kwa sababu wenzetu wamejua madhaifu yetu, tumepata nafasi hatukuzitumia, wenzetu wamezitumia, nadhani kocha ataenda kurekebisha."

Timu kama imeshinda pia kuna maneno yao ambayo kila atayekuja kuhojiwa tarajia mchezaji ataongea hivyo hivyo kana mwamba wamekaririshana.

Lakini siyo kwa Che Malone. Ana uwezo mkubwa sana wa kujieleza. Nadhani si kwa Simba tu, bali klabu zote. Wasichague manahodha kwa sababu ya uzawa. Wenzetu walioendelea kisoka na walioanzisha mchezo huo hawajaanzisha kuwa na kepteni uwanjani kwa sababu ya kuvaa kitambaa tu, au kuwa na uwezo wa kucheza soka, bali ni vitu vingi, ikiwemo kutuliza wachezaji, kuwakumbusha majukumu, kuwafokea ikibidi, kuwalinda na kuwatetea kama kaka au baba wakiwa uwanjani na madhila yote yatakayowakuta na mengine yanayofanana na hayo.

HABARI KITAIFA

# ... Aipa tano TTB kutangaza utalii

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, ameipongeza Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) kwa jitihada za kutangaza vivutio vya utalii nchini.

Pia amesisitiza kuwa juhudi hizo ni maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutekeleza falsafa ya 4R inayojikita katika Maridhiano, Ustahamilivu, Mageuzi na na Kujenga Upya Taifa.

Waziri Chana aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya kikazi katika Ofisi za TTB, jijini Dar es Salaam.

"Nawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kuitangaza nchi lakini nasisitiza lazima muwe na ushirikiano katika taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ili twende kwa pamoja. Mwende uwandani na kuvijua vivutio vilivyoko katika taasisi zote," alisema.

Waziri pia aliweka bayana kuwa serikali inaitegemea bodi hiyo kuendelea kuingiza mapato hasa fedha za kigeni na kuitaka kutengeneza programu endelevu za muda mrefu za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi na kuhakikisha utafiti wa utalii unaotolewa unajulikana kwa taasisi zingine za serikali zikiwamo bunge na vyuo vikuu.

Mkurugenzi Mkuu wa TTB, Ephraim Mafuru, alisema bodi hiyo imejikita katika vipaumbele kadhaa ikiwamo kuhakikisha uendelevu wa kifedha wa taasisi hiyo kwa kuwekeza kwenye mali za TTB na kuzalisha mapato kupitia Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali (DDMCC).

Pia alisema TTB itajikita katika kutengeneza mgawanyiko wa kikanda wa maeneo ya vivutio vya utalii na kubuni mazao mapya ya utalii kama 'Boat Cruises' sambamba na mbinu mpya za kutangaza utalii pamoja na kushawishi waendeshaji wa biashara ya utalii kuhusu namna bora ya kuandaa vifurushi vya utalii ili kupata wageni wengi zaidi.



Naibu Spika wa Baraza la Uwakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma (wa pili kushoto), Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (wa pili kulia) na Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa (kulia), wakisikiliza maelezo kutoka kwa Kamishna Msaidizi wa Uendelezaji wa Madini, Ally Samaje, walipotembelea maonesho kabla ya kufunga mkutano wa Kimataifa wa Madini na Uwekezaji, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Waziri atamba lengo la idadi watalii milioni tano kutimia

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, amesema mpaka kufikia mwaka 2025 serikali ina uhakika wa kutimiza lengo la kuongeza idadi ya watalii na kufikia milioni tano huku mapato nayo yakifikia dola bilioni sita.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya kutia saini makubaliano baina ya Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) na Chuo cha Mafunzo cha Italia (ENAIP).

Alisema hatua hiyo ya kuongeza watalii na fedha za kigeni itakwenda sambamba na kuimarisha huduma mbalimbali za watalii kama miundombinu na ujenzi wa hoteli za kisasa.

"Leo tunashuhudia mkubaliano kati ya NCT na Italia ambayo yatatusaidia kuongeza ujuzi kwa upande wa utalii wa mapishi ya vyakula vya aina mbalimbali na lugha ya kiitaliano," alisema.

Alisema makubaliano hayo ni muhimu sana kwa taifa kwani yatawapa ujuzi muhimu vijana wa Tanzania na alimshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza mchango wa sekta ya utalii kwenye pato la taifa mpaka kufikia asilimia 16.

Alisema Italia na Tanzania zimekuwa na uhusiano mzuri sana wa kiuchumi kwa miaka mingi na kusainiwa kwa makubaliano hayo ni ushahidi wa kutosha kwamba ushirikiano huo unaendelea kuimarika.

Mkuu wa NCT, Dk. Florian Mtey, alisema ushirikiano huo utakinufaisha chuo chake kwenye eneo la mafunzo ambapo wanatarajia wakufunzi wa chuo hicho wataenda kujifunza kwenye vyuo vya Italia.

Alisema wakufunzi watajifunza programu mbalimbali za masuala ya utalii na ukarimu pamoja na kujengewa uwezo kwenye masuala ya utafiti na namna ya kuandika miradi.

"Kwenye eneo la utafiti wa pamoja NCT na ENAIP tutafanya tafiti mbalimbali za kutuwezesha kutoa ushauri wa kitaalam kwenye sekta binafsi na sekta ya umma na wakufunzi wetu watabobea kwenye sekta mbalimbali baada ya kujengewa uwezo," alisema.

Pia alisema wanafunzi wa NCT watakuwa wakienda Italia kusoma kwenye vyuo mbalimbali vya nchi hiyo kujifunza kwa vitendo na kwamba tayari wakufunzi wanaosoma mapishi kutoka nchini Italia wameshaanza kuingia Tanzania. "Kuna wapishi wa Italia ambao tayari wako nchini na wanatoa mafunzo ya mapishi kwa wanafunzi wetu na watatusaidia wanafunzi wetu kubobea kwenye masuala ya mapishi," alisema

Alisema NCT kwa kushirikiana na ubalozi wa Italia nchini Tanzania wanatarajia kuanzisha mafunzo ya lugha ya kiitaliano chuoni hapo kwani kinasoko kubwa kutokana na ongezeko kubwa la watalii kutoka nchini Italia.

# RC: Uimarishaji mpaka ishara ujirani mwema

**Na Munir Shemweta,**
KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, amesema uimarishaji mpaka wa kimataifa baina ya Tanzania na Burundi ni ishara ya ujirani mwema na undugu kati ya serikali na wananchi.

Amesema Tanzania na Burundi zina mambo mengi ya ushirikiano yakiwamo kibiashara, uwekezaji, uchumi na kidiplomasia, hivyo uwapo kikao cha pamoja ni matokeo ya ushirikiano mzuri.

Aliwapongeza marais wa nchi hizo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan wa Tanzania na Evariste Ndayishimiye wa Burundi kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika kudumisha ushirikiano.

Andengeye amesema hayo juzi wakati akifungua Kikao cha Pamoja cha Kamati ya Wataalamu (JTC) kati ya Tanzania na Burundi kilichofanyika mkoani hapa.

"Tunapaswa kusimamia uimarishaji mpaka baina ya nchi zetu ili kudumisha ushirikiano mwema na undugu," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa aligusia pia suala la usafirishaji na kuweka wazi kuwa sekta hiyo imeendelea kuimarika kutokana na ushirikiano wa nchi hizo yakiwamo makubaliano ya mkakati wa ujenzi wa reli kutoka Uvinza- Kigoma hadi Msongati- Burundi.

Alisema ujenzi wa reli hiyo pamoja na mambo mengine, utaufungua mkoa wa Kigoma sambamba na kuiwezesha Burundi kukuza uchumi wake kutokana na kurahisisha usafirishaji bidhaa jambo alilolieleza kuwa litakuza sekta za biashara, viwanda na uwekezaji kwa ujumla.

Kiongozi wa Timu ya Wataalamu kutoka Burundi, Meja Jenerali Mbonimpa Maurice, alikielezea kikao hicho kuwa utawawezesha wataalamu wa nchi hizo mbili kujadili kwa kina changamoto zilizojitokeza kwenye suala la mpaka wa kimataifa.

"Mipaka ipo lakini changamoto zinatokea, hivyo tutakaa na kujadili changamoto hizi kwa lengo la kuimarisha mpaka wetu kwa manufaa ya nchi hizi mbili," alisema.

Mkutano wa uimarishaji mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Burundi, ulitarajiwa kumalizika jana ambapo Pamoja na mambo mengine, wataalamu walitembelea vijiji vya Bukililo na Nyakayenzi upande wa Tanzania na kijiji cha Kamusha nchini Burundi kwa lengo la kuangalia alama za mpaka.

Uimarishaji mipaka ya kimataifa ni utekelezaji wa makubaliano ya umoja wa Afrika kuwa ifikapo mwaka 2027 mipaka baina ya nchi za Afrika iwe imeimarishwa.

# DART yahamasisha matumizi kadi janja

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), umewataka watumiaji wa usafiri wa mwendokasi kuchangamkia kadi janja ili kupunguza usumbufu wanapotumia usafiri huo.

Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Athuman Kihamia, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu mwitikio wa wananchi katika matumizi ya kadi hizo.

Alisema kadi hizo ambazo zilianza kutumiwa Septemba mwaka huu zilibuniwa baada ya kuona utaratibu wa kutoa fedha taslim kwa wasafiri wanaotumia mabasi hayo ni wa usumbufu.

Utaratibu huo, alisema ni wa kisasa unaotumiwa maeneo mbalimbali duniani hivyo wananchi wanapaswa kuachana na utaratibu wa kizamani wenye usumbufu na kuhamia kidijitali zaidi.

"Sasa hivi ukinunua kadi janja kwa Sh. 5,000 unakuta imeshajazwa Sh. 3,000 ambazo unazitumia kwa nauli na uziri wa kadi hii ni kwamba unaweza kuchanja ukiwa kwenye mageti yaliyo njia kuu au ndani ya mabasi," alisema.

Alisema ili kuhakikisha wananchi wanaotumia usafiri huo wanapata urahisi wa safari yao DART ilinunua kadi 200,000 ambazo zinaendelea kununuliwa na watu wanaotumia usafiri huo na kwamba zimebaki chache.

"Tunashukuru sana kuona mwitikio umekuwa mkubwa watu wamekuwa wakinunua hizi kadi na tunaomba watu waendelee kununua tuondokane na utaratibu wa fedha taslim ambao unausumbufu sana," alisema.

Dk. Kihamia alisema Septemba, mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alizindua rasmi kadi janja na mageti janja ambayo yatafungwa kwenye vituo vyote vya mwendokasi.

Alipozindua kadi hizo na mageti, Mchengerwa alisema umefika wakati mwafaka kwa wananchi kutumia kadi janja na kuachana na utaratibu wa tiketi za makaratasi ambao umeshapitwa na wakati.

Pia aliwataka DART ishirikiane na wadau mbalimbali wa sekta binafsi kuhakikisha njia ya Mbagala inakuwa na mabasi 500 mpaka kufikia mwezi Desemba mwaka huu kwani njia ya mabasi hayo imeshakamilika.

Alisema hata njia ya Kimara Posta inapaswa kuongezewa mabasi hadi kufikia 170 kwani mabasi yaliyopo sasa hayatoshi na abiria wamekuwa wakilalamika kuchelewa vituoni kwa muda mrefu.

Waziri alisema kama UDART na DART hawawezi kuleta mabasi hayo basi washirikishe sekta binafsi ambayo alisema inauwezo wa kuleta mabasi mengi.




Mkurugenzi wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk. Athuman Kihamia akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akihamasisha wananchi wengi kutumia kadi janja kwenye usafiri mabasi hayo, ili kuwapunguzia usumbufu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kamati yatembelea mpaka wa Tanzania, nchi jirani Burundi

**Na Munir Shemweta,**
KASULU

KAMATI ya Pamoja ya Wataalamu ya Uimarishaji Mpaka wa Tanzania na Burundi (JTC), imetembelea Mto Malagarasi ambao ni sehemu ya mpaka wa kimataifa kati ya nchi hizo ili kujionea hali halisi ya eneo hilo.

Uamuzi wa kutembelea eneo hilo la mto Malagarasi ni sehemu ya programu ya kikao cha JTC kinachoendelea katika halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji mkoani Kigoma.

Kikao hicho pamoja na mambo mengine, kilipanga kutembelea katika vijiji vya Bukililo na Nyakayenzi upande wa Tanzania na kijiji cha Kamusha nchini Burundi.

Timu hiyo ya wataalamu ambayo kwa upande wa Tanzania iliongozwa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Upimaji na Ramani Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Samwel Katambi, huku upande wa Burundi ikiongozwa na Meja Jenerali Mbonimpa Maurice. Kamati hiyo ilitembelea eneo hilo la mpaka Niovemba 30, mwaka huu.

Lengo la kutembelea mpaka huo wa kimataifa ni kuwezesha JTC Kuandaa bajeti na mpango kazi wa uimarishaji mpaka wa kimataifa baina ya nchi hizo mbili.

Kikao cha Pamoja cha Wataalamu (JTC) kilichoanza kikao Novemba 18, kilitarajia kumalizika jana.

Uimarishaji mipaka ya kimataifa ni utekelezaji wa makubaliano ya umoja wa Afrika kuwa ifikapo mwaka 2027 mipaka baina ya nchi za Afrika iwe imeimarishwa.

# Waziri aridhishwa usimamizi fedha TASAF

**Na Lusungu Helela,**
SUMBAWANGA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, ameupongeza mkoa wa Rukwa kwa usimamizi bora wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia utekelezaji wa Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini kwa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi inayowanufaisha walengwa.

Sangu ambaye pia ni Mbunge wa Kwela mkoani Rukwa, alitoa pongezi hizo jana kwa nyakati tofauti alipotembelea kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na TASAF katika wilaya za Nkasi na Kalambo.

Aliitaja miradi hiyo inayotekelezwa na TASAF ikiwamo ujenzi wa kisima cha maji katika wilaya ya Nkasi pamoja na uanzishwaji wa shamba la miti ya mbao wilayani Kalambo.

Kuhusu ujenzi wa kisima hicho uliogharimu zaidi ya Sh. milioni tatu hadi kukamilika kwake, alisema kimekuwa msaada mkubwa kwa kuhudumia zaidi ya kaya 200 katika kijiji cha Kantawa

Kutokana na hatua hiyo, Sangu alimwekeleza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, kuhakikisha anawaleta wataalamu kutoka Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ili kukitambua na kukiboresha zaidi kwa kuwa kimeonekana kutiririsha maji katika kipindi chote cha mwaka.

"Jambo kubwa lililonileta hapa ni kufuatilia utekelezaji wa fedha za mradi wa TASAF. Mfuko huu umekuwa na programu mbalimbali zikiwamo zile zinazolenga kaya maskini ambazo hupokea fedha pamoja na shughuli za kujitolea ikiwamo ujenzi wa hiki kisima. Nimefarijika mno kujionea jinsi wananchi wanavyoisaidika kupitia kisima hiki," alisema Sangu

Katika hatua nyingine, Sangu alipongeza mradi wa upandaji miti ya mbao katika shamba lenye ukubwa wa ekari mbili uliogharimu Sh. milioni saba hadi kukamilika kwake. Mbali na miti hiyo kutarajiwa kutoa mbao, kwa sasa eneo hilo limekuwa kivutio kikubwa kutokana na hewa safi inayotokana na miti hiyo

Licha ya kupandwa miche 2,250 katika shamba hilo, Sangu alitoa wito kwa Mkuu wa Wilaya, Dk. Lazaro Komba, kuwaleta wataalamu kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ( TFS) ili kubaini chanzo cha tatizo kwa kuwa baadhi ya miche imeanza kunyauka.

Awali, Mbunge wa Kalambo, Josephat Kandege, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha fedha za TASAF zinawafikia walengwa na kuboresha maisha yao.

Baadhi ya wanufaika wa TASAF walieleza mpango huo ulivyowawezesha kuboresha maisha yao, ikiwamo kujenga nyumba, kusomesha watoto na kushiriki katika shughuli za maendeleo.





## CCM yasema haina mchezo uchaguzi Serikali za Mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Suzan Kunambi amesema Chama Cha Mapinduzi (CCM) hakidharau na hakitafanya mchezo katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu.

Amesema uchaguzi hu oni moja ya mikakati yao ya ushindi wa dola kwenye uchaguzi mkuu mwakani.

Akizungumza jana kwenye kampeni Kata ya Kilimani jijini hapa, alisema ni wajibu wa wanachama wa CCM kuhakikisha wananadi sera na mafanikio yaliyopatikana kwa kuwa chama hicho ndio chenye uwezo wa kuleta maendeleo, amani na mshikamano.

"CCM ni chama kinachoaminiwa na kimeleta maendeleo makubwa nchini, na haijawahi kudharau uchaguzi na hatutafanya mchezo huo, kushindwa kwetu ni mwiko kabisa niwaombe wananchi wa Kata hii ya Kilimani msidharau uchaguzi," alisema.

Aliwahimiza wananchi kujitokeza kupiga kura kwa kuwa ni muhimu kwenye kufanya maamuzi hata kama eneo husika lina mgombea mmoja wa CCM.

"Chama chetu kinaheshimu sana demokrasia na kina wagombea wazuri na wamepatikana kwa demokrasia katika michakato yetu ya ndani ya chama, hivyo siku ya kupiga kura usimuache yeyote mwenye sifa ya kupiga kura nyumbani, mnapaswa kubebana kwenda kupiga kura kuwachagua hawa viongozi wetu kiungo wanaofikisha changamoto zenu sehemu husika.

"Wanawake siku ya kupiga kura msianzishe ugomvi kwa waume zenu hakikisheni mnawabembeleza ili nao wajitokeze kwa wingi kupiga kura, tusifanye makosa kwenye mitaa, vijiji na vitongoji maana hii ndo mnasafisha njia ya kushika Dola 2025," alisema.

Naye mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Mtaa wa Chinyoyo wa chama hicho, Fausta Bendera, aliomba wananchi wamchague ili asimamie utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye eneo hilo ambayo kwa sasa inaendelea kujengwa ikiwamo shule ya msingi ili kuwaondolea adha wanafunzi kutembea umbali mrefu.

"Kwa kipindi kilichopita mmeona kazi niliyofanya katika eneo hili. Kwa miaka 40 tulikuwa hatujapimiwa ardhi yetu lakini nimefuatilia kwa muda mrefu na hatimaye serikali imetusikia na imetupimiwa.

"Kwa sasa tuna hati lakini katika maboresho tulitenga maeneo ya huduma za kijamii za shule, zahanati, kiwanja cha mpira naomba mnipe tena nafasi ili tufanikiwe kuwasilisha serikali kutatua kero hii," alisema.

# CBE, TCDC kusaidia ushirika kujiendesha kwa tija, ufanisi

**Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) kimeingia makubaliano na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kuvisaidia vyama vya ushirika nchini katika utunzaji wa kumbukumbu za fedha na kujiendesha kwa ufanisi. Mkuu wa CBE, Prof. Edda Lwoga, akizungumza kwenye hafla ya kutia saini makubaliano hayo jijini hapa juzi, alisema hali hiyo itasaidia vyama hivyo kutoa huduma bora kwa wanachama na kujiendesha kibiashara. "Makubaliano haya tunatumaini yatakwenda kuvisadia vyama vya ushirika zaidi ya 7,000 vilivyopo nchini kujiendesha kibiashara kutokana na kuwatumia wataalam wetu.

"Pamoja na wanafunzi walio kwenye mpango wa mafunzo kwa vitendo kwenda kwenye vyama hivyo kusaidia kutoa elimu ya mahesabu, utunzaji wa kumbukumbu pamoja na masuala mengine," alisema Prof. Lwoga.

Aidha, alisema CBE kwa kushirikiana na TCDC watavifikia vyama vyote vya ushirika na kuviwezesha mafunzo mbalimbali pamoja na kufanya utafiti ambao utabaini kero zilizopo ili kuzitafutia majibu ya kudumu.

"Wanafunzi wetu wanaokwenda mafunzo kwa vitendo kupitia makubaliano haya wataanza kuchukuliwa na vyama hivi vya ushirika kwenda kusaidia kazi mbalimbali ikiwemo utunzaji wa kumbukumbu na shughuli nyingine za kitaalam," alisema.

Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dk. Benson Ndiege, alisema tume hiyo imepewa jukumu la kusimamia vyama 7,200 nchini na kati ya hivyo asilimia 60 ni vyama vya kilimo na 40 ni vyama vya kifedha.

Alisema hivi sasa vyama vya ushirika vimewekeza katika vitu mbalimbali vikiwamo viwanda vya uchakataji wa bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo hivyo makubaliano hayo yatasaidia kuongeza tija na kujiendesha kibiashara.

"Juzi kuna chama cha ushirika kimezindua kiwanda kikibwa cha uchakataji wa bidhaa zitokanazo na mazao hivyo hapa kuna uhitaji mkubwa sana wa elimu kutoka kwa wataalam wa elimu ya biashara ili uwekezaji huu usiwe kazi bure ama mzigo kwa wanachama," alisema Dk. Ndiege.

Pia alisema ushirika unagusa sehemu kubwa ya wananchi hivyo yapo mahitaji makubwa ya kufanyika kwa utafiti ili kuboresha sekta hiyo nchini.

"Ushirika unahitaji sana utafiti hivyo mashirikiano haya ambayo tumeingia leo yatatusaidia kutumia wataalam wa CBE kufanya tafiti mbalimbali ambazo zitakwenda kuboresha vyama vyetu vya ushirika ili kujiendesha kibiashara na kuwakwamua kiuchumi wanachama wake," alisema.




Msimamizi wa Uchaguzi Jiji la Dodoma, Dk. Frederick Sagamiko, akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa na waandishi wa habari, jijini humo jana, wakati akiwapongeza kwa kuonesha ushirikiano mkubwa na kufanikisha mchakato wa uandikishaji hadi kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mazingira wezeshi kuwekwa watoto mahitaji maalum

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MKUU wa Wilaya ya Chamwino, Janeth Mayanja, amesema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalumu wanapata elimu bila kikwazo.

Mayanja aliyasema hayo wilayani hapa juzi baada ya kukabidhiwa vifaa vya ujenzi wa jiko katika Shule ya Msingi ya Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu Buigiri, vilivyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika.

Alisema serikali itahakikisha inashirikiana na wadau mbalimbali wa elimu katika kuunga mkono kazi ilivyofanya kwa NBS ambayo imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa jiko la kupikia chakula cha wanafunzi hao na walimu.

Kutokana na mchango huo, alisema serikali ya wilayani itahakikisha mchango huo unafanya kazi iliyokusudiwa na ujenzi utakamilika kwa wakati ukizingatia kuwa kila kitu kipo.

"Mimi kama mkuu wa wilaya kwa kushirikiana na watendaji wangu,nitahakikisha ujenzi wa jiko hili unakamilika ukizingatia kila kitu kipo na hata fedha ya kuwalipa mafundi ipo hivyo naomba likamilishwe haraka kama ilivyokusudiwa," alisisitiza. Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema katika kuadhimisha Siku ya Takwimu Afrika, wameamua kutoa mchango wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa jiko kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu Buigiri "Tumetoa vitu vyenye thamani ya Sh. milioni 3.9 na tumeamua kuja kuungana na watoto wetu kuhamasisha matumizi ya takwimu katika kupanga mipango mbalimbali ya Maendeleo," alisema.

Mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo, Yohana John, aliishukuru NBS kwa kuona umuhimu wa kuwatembelea na kutoa mchango kwa ajili ya ujenzi wa jiko litakalowasaidia kuboresha mazingira ya uandaaji wa chakula ambayo yalikuwa si rafiki.





## SMZ kuweka mazingira bora utekelezaji miradi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi kubeba jukumu la kuweka mazingira bora, yatakayosaidia utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo, ikiwamo inayofadhiliwa na taasisi za kimataifa, ili kuongeza kasi ya maendeleo kwa maslahi ya uchumi wa nchi.

Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman alisema hayo alipokutana na viongozi wakuu wa taasisi ya kimataifa ya Kukuza Elimu ya Mazingira Duniani (Foundation of Environmental Education - FEE) katika mkutano uliofanyika Hispania.

Othman alisema serikali ya Zanzibar, imeshaonesha utayari wa kutekeleza wajibu huo, ili kufanikisha miradi hiyo muhimu, kwa ajili ya uchumi wa nchi.

Alisema lengo la safari yake ya Hispania ni kushiriki vikao na mkutano wa Dunia wa Shirika la Kimataifa wa 'The Sun and Blue Congress', kuwapo sera bora, sheria makini na hitaji la sasa la Zanzibar kufanikisha mipango yake ya maendeleo kupitia uimarishaji wa utalii, utunzaji wa mazingira, na mikakati katika kujenga uchumi wa buluu, ni sehemu ya wajibu huo.

Pia alisema baada ya kurejea Zanzibar, watahakikisha wanaandaa mikakati madhubuti ili utekelezaji wa hatua za miradi hiyo, unaanza mara moja.

Mkutano huo umeafiki makubaliano ya msingi ya kuisaidia Zanzibar katika nyanja mbalimbali, zikiwamo za ulinzi wa mazingira, uchumi wa buluu, elimu ya utunzaji wa mazingira, mpango wa shirika la kimataifa la 'Blue Flag' na ulinzi wa viumbe vya baharini.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema serikali kwa sasa inaamini juu ya uwekezaji unaozingatia maslahi ya jamii, utamaduni, na uhusika wa moja kwa moja wa asasi za kiraia, ili kuhakikisha umma unafaidika na hatua zote za maendeleo.

Daniel Schaffer, Mkurugenzi Mtendaji wa FEE, alishukuru hatua ya Othman na ujumbe wake kuitembelea Hispania ili kuhudhuria mkutano huo wa kimataifa, pamoja na kuonesha utayari wa kufanyakazi kwa mashirikiano na taasisi yake, kwaajili ya mafanikio ya pande zote.

Alisema kutokana na uzoefu wake wa takriban nchi 85 ambazo taasisi yake inazihudumia kwa kutoa misaada mingi ya maendeleo, anazielewa changamoto zinazokabili jamii, hasa za mataifa yanayoendelea, ikiwamo Zanzibar.

Alitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na urasimu, ukosefu wa dira na moyo wa kujitolea, pamoja na uzito wa mrejesho katika mawasiliano, ambazo ni kikwazo cha mashiriano, katika kufanikisha maendeleo, hasa ya misaada kutoka taasisi za kimataifa.

Aliishauri Zanzibar kujenga umakini na kujenga ufanisi ili kutumia fursa nyingi zilizoko katika taasisi yake na kuutumia uzuri wa asili wa nchi hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema yeye na wenzake walikwisharidhia kuendelea kusaidia katika kuimarisha sekta mbalimbali zikiwamo za utalii na mazingira pia kwa kusaidia kujengea uwezo kiuchumi.

# RC ataka elimu uzalishaji bidhaa bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Massoud, amezitaka taasisi zenye dhamana ya kusimamia wajasiriamali visiwani Zanzibar kuwapa miongozo namna ya kuzalisha bidhaa zao.

Pia amezitaka taasisi hizo kuwapa elimu jinsi ya kuzifikia fursa za upatikanaji wa mikopo inayotolewa.

Amesema hatua hiyo itasaidia kasi ya uzalishaji wa bidhaa zao lakini pia kupata mikopo kwa ajili ya kuendeleza biashara zao za kujikwamua kiuchumi.

Mattar aliyasema hayo kisiwani Pemba wakati akifungua mafunzo wa wajasiriamali kuhusu program ya Imarisha Uchumi na Mama Samia ambayo ina manufaa makubwa katika kuimarisha uchumi wa wananchi wenye kipato cha chini na kujikomboa na umaskini.

Alisema kuwapatia mikopo bila kuwapa elimu, watashindwa kufikia lengo lililokusudiwa ikiwamo kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini wa kipato.

Kwa mujibu wa Mattar, kuna baadhi ya wajasiriamali wanapatiwa mikopo lakini hawarejeshi na sababu kubwa ni kukosa elimu ya kuendesha shughuli zao ipasavyo.

Mattar alisema uanzishwaji wa Baraza la Uwezeshaji Kiuchumi Tanzania pamoja na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar lengo ni kusimamia na kuhakikisha wanawasaidia wananchi kiuchumi ili kuongeza kipato.

Pia alisema kuna malalamiko mengi kut9oka kwa wananchi kutopata mikopo, hivyo alizitaka taasisi za kifedha zinazopewa dhamana ya kutoa mikopo kwa wananchi kuondoa urasimu, masharti makubwa ya kuwabana ili kupata mikopo kwa unafuu.

Naye Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, alisema ili Tanzania ifanikiwe lazima maisha ya wananchi yawe mazuri, hivyo program ya AMASA ina lengo la kuwasaidia wajasiriamali kufanya shughuli zao kwa ubora, kuzitumia fursa zinazotolewa na serikali ili kupiga hatua kimaendeleo.

"Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia haitamwacha mtu nyuma. Itahakikisha inawafikia walengwa ili kupiga hatua. Niwaombe wananchi mjisajili kwenye mfumo wa IMASA ili serikali kutoa taarifa kamili kwa maendeleo zaidi," alisema. Mkurugenzi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEA), Juma Burhan, aliwataka wananchi na wajasiriamali kujiepusha na mikopo ya kausha damu ambayo ina riba kubwa na hupelekea kushindwa kufanikiwa katika uendeshaji wa biashara zao.

Alisema ni vyema kuitumia fursa ya mikopo inayotolewa na serikali ambayo haina riba na urejeshaji wake hauna vikwazo tofauti na mikopo ya kausha damu ambayo ni changamoto kubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Mkurugenzi huyo alisema ZEA imeshatoa mikopo ya Sh. bilioni 33 kwa Zanzibar na kuwafikia watu 27,973, hivyo kuwataka wote waliopata fursa hiyo kufanya marejesho kwa wakati ili kutoa nafasi kwa watu wengine kupata mikopo.




Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Zanzibar, Zuberi Chembera (kulia), akikabidhi zawadi ya karafuu kwa Balozi Mteule wa Korea Kusini, nchini Tanzania, Eunju Ahn, wakati balozi huyo, alipokutana na Maofisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi Kamisheni ya Zanzibar, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zanzibar yapewa somo kuporomoka jengo Kariakoo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ADA TADEA kimesema Zanzibar inaweza kujifunza baada ya jengo la ghorofa kuporomoka Kariakoo jijini Dar es salaam kwa kuweka utaratibu wa kuyakagua majengo yote visiwani hapa kuyafanyia uhakiki ili kunusuru majanga yanayoweza kujitokeza.

Mkurugenzi wa Uchaguzi Chama hicho, Ali Makame Issa, aliyasema hayo visiwani hapa jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kutoa pole kwa Watanzania baada ya kutokea maafa ya kuanguka kwa jengo huko Kariakoo.

Alisema Zanzibar inajenga majengo mbalimbali ya ghorofa yakiwamo ya hospitali na shule, hivyo hatua hiyo itasaidia kuona majengo hayo kama yamekidhi vigezo na ubora wa kuwapo kwake ikiwamo hali ya usalama.

"Serikali yetu isisubiri mpaka itokee ajali kama iliyotokea Kariakoo. Ni vizuri na sisi kuanzisha utaratibu wa kuyapitia majengo yote ya ghorofa mapema ili kujiridhisha kama kuna usalama katika majengo haya," alisema.

Pia alisema namna ya kupitia majengo isiwe tu pale jengo linapoanguka bali kuwe na utaratibu wa kudumu wa vipindi maalum kuhakikisha yanakaguliwa kila wakati.

"Tunaamini SMT imeshatangaza kwamba majengo yatafanyiwa uhakiki. Kuna wengine wanaweza kufanya haraka kuyakarabati ili wanapopita wataalamu yaonekane yako salama," alisema.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada anazozichukua katika kulisimamia suala hilo kuona majeruhi wanapatiwa matibabu na wale waliofariki wanasitiriwa.

Katika hatua nyengine, chama hicho kimewataka viongozi wa vyama vya siasa kujitathmini na kubadilisha maendeleo ya kisiasa ili kuhakikisha vyama vyao vinaweza kuaminika kwa watu na kufanya siasa za kidemokrasia.



**ZUCHU**
UKURASA 12





# 'NICE TO MEET YOU'

## Kiki iliyowarudisha Lulu Diva, Hemed PHD

TAMTHILIA ya 'Nice to Meet you' inayowakutanisha waigizaji Lulu Abas 'Lulu Diva' na Hemed Suleiman 'Hemed 'PHD' waliokuwa na uhasama imezinduliwa rasmi na kuwafanya kumaliza tofauti zao.

Wawili hao inasemekana walianza tofauti zao tangu walipokuwa lokesheni wakirekodi tamthilia hiyo iliyowahusisha na ugomvi wao kuendelea hadi kwenye maisha yao ya kawaida.

Lakini wameombana msamaha na kuendelea na maisha yao baada ya kumaliza tofauti zao hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari Hemed PHD alisema kuwa yeye ndio kinara wa tamthilia hiyo ya 'Nice to meet you'.

"Ushiriki wangu katika tamthilia hii mimi ndio mhusika Mkuu na nimeigiza kama mtumishi wa Mungu nimeigiza humo ndo unatakiwa kunifuatilia kuanzia uzinduzi rasmi hadi tamthilia yenyewe Watanzania wajiandae kumuona Saimon Mlokole." alisema Hemed

Kwa upande wa Lulu naye pia, amesema hakutaka kupishana na Hemed lakini ni tofauti za kibinadamu wao kupishana alioneshwa kuchukukizwa lakini kwa sasa wapo sawa na kuwataka mashabiki wafuatilie tamthilia hiyo.

BASI SAWA

## Mashabiki wamtaka Zuchu kutaja..




MASHABIKI wa muziki wanaendelea kumshinikiza Zuchu, kutaja jina la albamu yake mpya ambayo anaitangaza kwa kasi.

Zuchu ambaye yuko mbioni kutoa albam yake ya kwanza, yupo katika harakati za kuitangaza kwa kutambulisha baadhi ya nyimbo ambazo ziko ndani.

Baadhi ya watu walishiriki baadhi ya machapisho yake na kumueleza msanii huyo kutoka lebo ya WCB, kutoa jina kamili la Albam yake kwani wana hamu ya kuifahamu.

## Ibraah aomba aachie ngapi?



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Ibraah, amewapa kazi mashabiki zake kuchagua idadi ya ngoma wanazotaka aziachie kabla ya mwaka kumalizika.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Ibraah, amewataka wafuasi wake kuwa anasubiri kuona majibu yao ili aanze kazi ya kuachia moja hadi nyingine.

"Shabiki wangu namba moja na mimi mwenyewe nasubiri, niambieni niachie ngapi? Ibraah amewahoji mashabiki zake.



## SHAMSA AZIDI KUDEKA

WAIGIZAJI maarufu wa Bongo Muvi, Shamsa Ford na Mlilo, wanazidi kutamba katika maisha yao ya ndoa, baada ya kuachia video yao fupi wakionyesha mahaba mazito yasiyo na kifani.

Kupitia ukurasa wa Instagram wa Mlilo, alichapisha video hiyo ikiwaonyesha wawili hao wakijadili namna ya kusalimiana wakati wa kulala usiku na wanapoamka.

"Kila siku tunapoamka unaniambia habari za asubuhi, mimi naona salam yako ni nzito kushinda maisha yangu, siwezi mume wangu," amesikika Shamsa Ford akisema huku akideka.





## Aslay arudi tena

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Aslay, amesema wakati umefika wa kurudi tena katika kilele cha muziki na kuwataka Watanzania kusubiri mambo mapya kutoka kwake.

Ujumbe aliouchapisha katika ukurasa wake wa Instagram, Aslay amesema safari yake imekuwa ndefu iliyojaa milima na mabonde, lakini kipindi cha furaha yake kimerejea tena.

"Napenda kumshukuru Mungu kwa uzima wangu na kipaji alichonipa, kwa familia yangu , ndugu zangu na marafiki zangu kwa kuniunga mkono na dua zenu na kuwa na mimi wakati wote wa maisha yangu. Ni kwa furaha na moyo wa amani naweza kukiri Aslay amerudi rasmi kwenye kilele cha muziki," amesema Aslay.

## NGOMA 5 ZA KALI ZA KING KIKI

**Na Adam Fungamwango**

MBUYU umeanguka. Ndiyo unavyoweza kusema baada ya Tanzania kupata msiba mkubwa kuondokewa na mwanamuziki mkubwa, Kikumbi Mwanza Mpango, King Kiki, aliyefariki usiku kuamkia Novemba 15, nyumbani kwake Mtoni kwa Aziz Ally, jijini Dar es Salaam.

Aliagwa  Jumatatu iliyopita viwanja wa Leaders, jijini Dar es Salaam na kuzikwa siku hiyo hiyo kwenye Makaburi ya Kinondoni.

Mwanamuziki huyo alikuwa mwimbaji na mtunzi alizaliwa Januari Mosi, 1947, Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, akaja nchini na kuwa mwanamuziki maarufu hasa nchini akiwa na bendi mbalimbali.

Leo tutaziangalia nyimbo tano ambazo zilimpatia umaarufu mkubwa, na kuwa mmoja wa mastaa wakubwa hadi anafariki dunia.

### Kasongo Rudi Nyumbani

Ni wimbo maarufu sana uliorekodiwa katikati ya miaka ya 1970, akiwa na bendi ya Maquiz du Zaire. Ni wimbo ambao kila shabiki wa muziki Tanzania aliupenda na kuanza kumfahamu, na kumfuatilia mwanamuziki huyo.

"Wanasema urudie Kasongo, kwenye natoka kunawake moto." Ni moja kati ya nyimbo bora kabisa za mwanamuziki huyo.

### Nimepigwa Ngwala

Huu pia ni utunzi wake, ulitoka kwenye albamu moja na 'Kasongo'. Ni moja ya nyimbo zilizomuweka Kiki kwenye ramani ya muziki na kuwa mmoja wa mwanamuziki bora kabisa nchini.

Wimbo huu unamzungumzia mtu aliyekuwa akimfuata mpenzi wake, lakini kumbe kuna watu wana wivu, wanamvizia na kumpiga ngwala, wakiwa hawapendi jinsi anavyomfuatafuata, kwani mwanamke anawakataa wao na kumkubali yeye.

### Anjelu

Wimbo huu haukutungwa na yeye, badala yake ulitungwa na marehemu, Kasongo Mpinda, lakini Kiki akiimba kwa hisia kali na kuwa moja ya wimbo bora kabisa.

Wimbo huu ulimfanya marehemu Dr Alex Khalid, mmoja wa wanasiasa na wafanyabiashara maarufu wakati huo kumpa vyombo vya muziki na akaanzisha bendi ya Orchestra King Kiki Double O.

### Kitoto Kaanza Tambaa

Wimbo huu aliutunga na kuimba akiwa na bendi yake ya Orchestra King Kiki Double O, uliondokewa kupendwa mno hata na kizazi cha hivi karibuni ambao baadhi ya wanaojifunza muziki na kwenye mashindano mbalimbali, ulitumiwa kwa ajili ya mtihami wa kuimba.

### Kitambaa Cheupe

Sina haja ya kuuelezea sana wimbo huu, kwani vijana wengi wa kizazi cha sasa wanamfahamu mwanamuziki King Kiki na wimbo huu wa 'Kitambaa Cheupe', alioutunga akiwa na bendi ya Capital Wazee Sugu, na ulirekodiwa nchini Uingereza walipokwenda kwenye ziara.



FILAMU

# Nje malaika, ndani shetani

**Na Adam Fungamwango**

HAPA duniani kuna baadhi ya watu ambao ukiwaona kwa macho ya kawaida tu, unaweza kudhani kuwa ni watu wema na wacha Mungu.

Lakini nyuma ya pazi wamebeba vitu vizito ambavyo huwezi ukadhania. Ni wanyama, makatili na kila aina ya uzandiki.

Filamu ya 'Chini ya Jua' imebeba ujumbe mzito ambao unakuwa ni fundisho kwa watu wenye tabia kama hizo.

Kundi la watu wasiojulikana walikuwa wakimuua binti mmoja ambaye ni denti wa chuo. Binti mwingine wa chuo aitwaye Ritha alikuwa akipita porini ambapo ndiyo njia ya kuelekea chuo na kukuta mwenzake 'ametaitiwa' na wauaji akalipiga picha tukio hilo. Kwa sababu ni mtoto wa kike, alishindwa kuvumilia kuona denti mwenzake anauawa, akapiga kelele, kamera ikaanguka chini, akakimbia.

Baada ya kuua, watu hao wakaanza kumkimbiza mtu ambaye alipiga kelele. Jitihada zao zilifanikiwa, wakamkamata na kumchimbia shimo refu wakamzika ardhini akiwa amesimama wima na kubakisha kichwa tu.

Baada ya mateso makali, wakamuacha hapo wakidhani atakufa. Kijana mmoja wa kijijini aliyeitwa Bahati alipita hapo na kumfukua, akampeleka nyumbani kwake.

Baada ya matibabu, na chakula kwa wiki nzima, hali ya Ritha ikatengemaa.

Rafiki yake Pamela anasambaza ujumbe kwenye magrupu yote na kuanza kusakwa binti huyo ambaye alikuwa akitoka Dar kwenda Tabora chuoni, lakini hakufika na amepotelea kusikojulikana.

Pamela  aliyesambaza ujumbe naye anauawa na wasiojulikana.

Hatimaye baada ya msako wa muda mrefu, Ritha anapatikana. Mwenyewe Ritha baada ya kurejea kwao, anamwambia mama yake kuhusu hali ya kijana bahati kule kijijini akiwa na mama yake ambaye ni mgonjwa wa akili.


Ritha aliondokea kumpenda kijana Bahati, hivyo alijitolea kumtoa kijijini na kumleta mjini, akimtibia pia mama yake hadi akapona.

Baada ya kupona, mama Bahati akakaribishwa nyumbani kwa akina mzee Honchi ambaye ni baba wa Ritha.

Hata hivyo mzee Honchi na mama Bahati wanakataa watoto wake wasioane. Inakuja kudhihirika kuwa ni mtu na dada yake.

Kumbe huko nyuma, mzee Hochi aliwahi kuwa na mahusiano na mama Bahati hadi kumpa mimba, lakini akakataa kwa sababu ana mke tayari. Ndipo alipozaliwa Bahati.

Tukio hilo linawakasirisha wote mle ndani, na kabla chochote hakijaendelea inajulikana kama kumbe pia mzee Honchi ndiye aliyewatuma vijana wasiojulikana kuuua msichana wa chuo ambao nusura pia amtoe roho binti yake Ritha. Ni kwamba msichana yule alitishia kuanika kwa sababu alimpa ujauzito ambao hataki kuulea, hivyo kuficha siri akataka auawe.




Kama vile haitoshi, alipobanwa, mzee Honchi alikiri kuhusika na kifo cha Pamela, ambaye alimuua kwa mkono wake akidhani anaficha siri baada ya kupotea, akidhani kuwa huenda yuko kwa bwana, lakini anajifanya hajui.

# Denzel haachi pombe

MWIGIZAJI mkongwe wa filamu za Hollywood, Denzel Washington, amesema hawezi kuacha kunywa mvinyo hadi atakapofikisha umri wa kuitwa kikongwe.

Wakati wa mahojiano na jarida la Esquire, mshindi huyo wa tuzo ya Academy mara mbili, alisema alianza kunywa kinywaji hicho tangu 1999 wakati alipojenga nyumba yake ya kwanza na hawezi kuacha ghafla kama wanavyofikiria watu wengine.

"Tulijenga nyumba hii kubwa mwaka wa 1999 na mpaka sasa kuna chupa elfu kumi za mvinyo, nilijifunza kunywa na nitaendelea kwa miaka yangu ya '61 hadi 82," amesema Washington.





## Rema, Kuti kupamba Coachella

ORODHA ya wasanii watakaotumbuiza tamasha kubwa la muziki duniani la Coachella imetolewa, huku wasanii wa Nigeria wakitamba kuwa miongoni mwa wanamuziki watakaotumbuiza.

Tamasha hilo linalofanyika kila mwaka na kuwavutia maelfu ya watu wanaokusanyika katika Klabu ya Empire Polo iliyoko California, majina ya wasanii wa Afrika Rema na Seun Kuti, yakitajwa kuwa miongoni watakaopanda jukwaani kutoa burudani mwaka unaokuja.

Seun Kuti atakuwa amevunja rekodi kwa kuwa msanii wa kwanza kutoka Afrika aliyepanda jukwaa hilo mara nyingi, kwani atakuwa ametumbuiza mara tatu tangu 2012.

## Kendrick Lamar kinara Hip hop

MTANDAO wa kuuza wa Apple, umemtaja, Kendrick Lamar kuwa kinara wa wanamuziki wa hip hop kutokana na na kuuza nakala nyingi za nyimbo duniani.

Kendrick Lamar ambaye ana tuzo nyingi za Grammy na Drake wanashindana kwa kufikisha kiwango cha juu cha mauzo, Wimbo wa 'Not Like Us' umefanikiwa kushika namba moja katika chati za Billboard za nyimbo 100 bora.

Msanii huyo ametawazwa kuwa Msanii Bora wa Mwaka wa Muziki wa Apple na kuwatupa washindani wake Future, Kanye West, TY Dolla $ign, na Tyler the Creator.





## Chike umewachanganya ujue

MASHABIKI wa mwanamuziki Chike, wamejikuta wakichanganyikiwa baada ya msanii huyo kuchapisha picha akiwa na mwanamke aliyejificha sura yake.

Juzi, Chike alichapisha picha hiyo katika ukurasa wake wa Instagram ikiambatana na picha hiyo ikimwonyesha mwanamke huyo sehemu ya mgongoni huku kichwa chake akiwa amekiegesha katika bega la mwanamuziki huyo.

Chike akiwa amevalia vazi la kitamaduni la Igbo na mwanamke huyo akivalia vazi la Kiyoruba, na kisha aliandika "Ninapoamka asubuhi, namshukuru Mungu kwa ajili yako,".

## Mtoto wa Beyonce azua jambo Nigeria

VIDEO inayosambaa mitandaoni inayomwonyesha mtoto wake Beyonce, anayeitwa Blue Ivy akiwazuia wazazi wake wasiondoke baada ya kutajwa jina la Burna Boy, umeibua gumzo nchini Nigeria.

Blue Ivy na wazazi wake walikuwa wakitoka nje wakati sherehe za utoaji tuzo za 66 za Grammy ziliyofanyika miezi kadhaa iliyopita. Walipokuwa wakinyanyuka mwongozaji wa sherehe alimtaja Burna Boy kuwa mwanamuziki anayefuata kutumbuiza, ndipo Blue Ivy alipoonekana kuwazuia wazazi wake wasitoke.

Kutokana na hatua hiyo, Wanigeria wengi wameonekana kufurahishwa na kitendo hicho wakieleza ni alama tosha kuwa wasanii wao wanatambulika duniani kote.





# CHADEMA yaja na operesheni 'Ondoa Mizigo'

**Na Mary Mosha,** MOSHI

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa Kilimanjaro, kimetangaza kuanzisha operesheni maalumu ya Ondoa Mizigo Moshi, ambayo itawaondoa madarakani viongozi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji wanaolegalega katika shughuli za maendeleo.

Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Kilimanjaro, Basil Lema, alitangaza kuja kwa operesheni hiyo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya chama hicho katika Kata ya Njoro na kwamba operesheni hiyo itasaidia kuleta mandeleo na uwajibikaji kwa viongozi.

Alisema katika kipindi cha miaka minne, kumekuwa na matatizo mengi ikiwamo kuwa na baadhi ya viongozi mizigo.

"Tujitokeze kwa wingi kupiga kura ili kuondoa mizigo inayoshindwa kutekeleza majukumu yao. Agizo la pili, wananchi kuanzia Novemba 20, hadi siku ya uchaguzi, ni jukumu letu kupita nyumbani kwa nyumba, mtaa kwa mtaa, kuomba na kupiga kura ili kuhakikisha tumepata viongozi bora na wawajibikaji," alisema Lema.

Alisema kuendelea kuacha kuhamasisha na kuombeana kura, kutasababisha kukosekana kwa haki na kuendelea kupitia matatizo ya ugumu wa maisha.

"Tatu, ni wajibu wetu kuhakikisha mara baada ya kupiga kura kusogea mita 100 na kuendelea kulinda kura, ili kupata majibu yaliyo sahihi. Hakuna kutishika na kuhofia katika kulinda haki zetu," alisema Lema.

Meya wa zamani wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, akizungumza katika kampeni hiyo, aliviomba vyombo vya usalama pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza uuzaji wa maeneo ya wazi na matumizi mabaya ya rasilimali za manispaa hiyo.

"Ziko taarifa kwamba baadhi ya rasilimali za Manispaa ya Moshi, ikiwamo mitambo ya kutengenezea barabara, iko mikononi mwa vigogo na inafanya shughuli binafsi. Hii si sawa kwa ustawi wa wana Moshi," alisema Mboya.

Mmoja wa wanachama wa CHADEMA, Sebastian Nnko, alisema kurejea kwa hamasa za CHADEMA katika Manispaa ya Moshi, kutarudisha mji kuwa safi na stendi mpya Ngangamfumuni itakamilika.

Naye , Hawa Mdee alisema kwa sasa mji wa Moshi unatishiwa na uchafu, huku akilalamikia magari yanayokusanya taka kuwa chakavu na vijana hawana vitendea kazi.

"Watu wapo kwa maslai yao. Hatuogopi kusema ukweli ila bado chama tawala hawakujiandaa kuipata Manispaa na badala yake walipewa kama zawadi, hivyo, hawajui kutunza na sisi kama wana Moshi hatutakubali,"alisema Anna Mrema.




Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Meneja Mkazi wa Airfrance, Rajat Kumar baada ya kuhutubia hafla ya uanzishwaji wa safari ya moja kwa moja kati ya Ufaransa hadi Mkoa wa Kilimanjaro, jijini Arusha, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwenyekiti mpya EAC kujulikana Nov. 30

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HATIMA ya nani atakayeshika nafasi ya Uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kujulikana Novemba 30, mwaka huu, jijini Arusha kwenye mkutano wa kawaida wa wakuu wa nchi wanachama.

Akizungumza jana jijini hapa, Mkuu wa EAC, Veronica Nduva, alisema wakuu wa nchi watakapomaliza mkutano wao wa ndani, wataamua nani kati yao atashika nafasi ya mwenyekiti wa EAC kwa muda wa mwaka mmoja.

"Wakuu wa nchi ndio watakaoamua nani atashika nafasi hiyo, lakini tunashukuru kwa ushirikiano unapelekea EAC kutimiza miaka 25 ya mtangamano tangu ilivyoanzishwa 1999," alisema.

Alisema Novemba 30, mwaka huu, jumuiya inafikisha miaka 25. Sherehe hizo zinaambatana na mkutano wa kawaida wa wakuu wa nchi wanachama wa EAC.

Kabla ya hapo, kutakuwa na mikutano mbalimbali ya mawaziri, wadau wa sekta mbalimbali, ikiwamo binafsi na maonyesho ya mavazi na vyakula tofauti.

Hivi sasa nafasi uenyekiti wa EAC inashikiliwa na Rais wa Sudan, Salva Kiir, ambaye alipokea kijiti hicho kutoka kwa Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye.

Alisema katika mkutano huo wa mawaziri na vikao vya juu Septemba 29 watajadili mambo manne ambayo ni uanzishwaji wa soko la pamoja,muungano wa fedha wa kisiasa na shirikisho la kisiasa ikiwemo amani na uhusiano katika ya nchi za EAC.

"Wakuu wa nchi wanachama watatuambia jumuiya yetu hadi sasa ipoje na tunaenda wapi, lakini pia mambo gani wanataka tuyawekee msukumo zaidi, hasa katika umoja wa forodha na mengineyo," alisema

# Chatanda ataka CCM kujitokeza Uchaguzi Mitaa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, ametoa rai kwa wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kuwapigia kura wanachama wao, katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu.

Chatanda ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, alisema hayo jana wilayani Karatu wakati akizindua kampeni za CCM Mkoa wa Arusha, katika uwanja wa Mazingira ulioko mjini humo.

"CCM tuna kila sababu ya kushika dola kwa sababu tumefanya kazi kubwa ya kuisimamia serikali, kutekeleza Ilani yetu ya uchaguzi na katika hili hatuna mzaha,"alisema,

Aidha, Chatanda alisema serikali imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha amani inatawala, ili wananchi wanendelee na majukumu yao ya kila siku ya kujiletea maendeleo. Katika hatua nyingine, Chatanda aliwapokea wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliaomua kujiunga na CCM kwa madai ya kuchoshwa na sera za chama chao, ambazo hazitekelezeki na wamekuwa wakihamasisha maandamano yenye nia ya kuvuruga amani.

Kwa mujibu wa Chatanda, sheria ya uchaguzi ya mwaka huu inakataza wagombea kupita bila kupigwa hivyo wagombea wote watapigiwa kura zikiwemo za 'ndiyo' na 'hapana' kwa wale ambao katika maeneo waliyogombea wagombea wa vyama vingine hawakujitokeza kuchukua fomu za kugombea.

"Msibweke katika maeneo ambayo wagombea wa vyama vingine hawakusimamisha wagombea.Nendeni mkafanye kampeni katika maeneo hayo na kuwahamasisha wakawapigie wagombea wetu kura zote za ndiyo,"alisema

Aidha, alisema uchaguzi huo ni muhimu sana kwa kuwa ni ngazi ya mwanzo wa taswira ya CCM kushika dola katika uchaguzi mkuu wa mwakani na hilo ndilo lengo la chama chochote cha siasa.

"Ushindi wetu katika uchaguzi huu ndiyo taswira ya ushindi wetu mwakani. Na sisi wanawake tujipange kikamili hivyo ushindi wa CCM mwaka huu ni ndiyo,"alisema.

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# King Kiki, mwanamuziki wa kwanza kumiliki Mercedes-Benz hapa Bongo

**Na Adam Fungamwango**



MAMIA ya Watanzania wakiongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Damas Ndumbaro, Jumatatu iliyopita walimiminika kwenye viwanja wa Leaders, jijini Dar es Salaam, kumuaga mwanamuziki maarufu na mkongwe nchini, Kikumbi Mwanza Mpango Mwema, maarufu kama King Kiki na kuzikwa siku hiyo hiyo kwenye Makaburi ya Kinondoni.

Mwanamuziki huyo alifariki dunia usiku wa kuamkia Novemba 15, nyumbani kwake Mtoni kwa Aziz Ally, jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa mtoto wake, Jesca Kikumbi, mwanamuziki hiyo alikuwa akisumbuliwa na tezi dume, pia saratani ilikuwa imepanda hadi kwenye ini.

Kwa msaada wa Serikali, King Kiki, alipelekwa nchini India kwa matibabu, na alikuwa kitandani kwa kipindi kirefu akiugua.

**KING KIKI NI NANI?**

Ni mwanamuziki, mwimbaji na mtunzi mahiri nchini, aliyekonga nyoyo za Watanzania wengi wa rika mbalimbali kuanzia watu wazima hadi watoto.

Nikisema hivyo ni kwamba watu wazima wanamfahamu kwa nyimbo zake alizotunga na kuimba akiwa na bendi ya Orchetra Fauvette, baadaye Maquis du Zaire, Orchestra Safari Sound, 'Masantula Ngoma ya Mpwita', Orchestra King Kiki Double O, Sambulumaa, Zaita Musica na Ya Capital, Wazee Sugu.

Vijana wa sasa wanamkumbuka mzee Kiki kwa ngoma yake inayochengua sehemu zote za burudani, 'Nzibola', lakini wenye wakiitambia kwa jina la 'Kitambaa Cheupe'.

**KUINGIA NCHINI**

Alizaliwa Januari Mosi, 1947, Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, baadaye akaondokea kuwa mwanamuziki maarufu hasa nchini akiwa na bendi mbalimbali.

Mara ya kwanza alifika nchini Tanzania akiwa na bendi ya Orchetra Fauvette mwanzoni mwa miaka ya 1970, akiwa na Freddy Ndala Kasheba na kutoa vibao mbalimbali kama 'Vivi', 'Nono na Kalimie', 'Zula' 'Jackline', lakini alirejea tena Zaire (sasa DRC), ambapo alikuja tena nchini katikati ya miaka hiyo, akijiunga na Maquis du Zaire, akatunga nyimbo nyingi kama 'Kasongo rudi Nyumbani', 'Maggie', 'Nimepigwa Ngwala'.

Alipata umaarufu mkubwa akiwa na bendi hiyo kiasi cha mashabiki kumpachika jina la King, yaani mfalme kutokana na tabia yake wakati huo ya akiwa anaingia ukumbini alikuwa amevaa joho kama refu kama mfalme, lakini pia anapoingia ukumbi mzima unasimama kwa ajili ya heshima yake kama mfalme mpaka anapopanda jukwaani ndipo kila mmoja ataendelea na shughuli yake.

Baada ya kupata umaarufu mkubwa akiwa na bendi hiyo, mfanyabiashara Hugho Kisima, ambaye alikuwa na bendi ndogo wakati huo, Orchestra Safari Sound ikitumia mtindo wa Nyekese, aliamua kuiboresha bendi yake kwa kujaribu kumnyakua.

**ANUNULIWA BENZ**

Haikuwa kazi ndogo kumshawishi kutoka Maquis du Zaire, hivyo moja ya vishawiki ilikuwa ni kumnunulia gari aina ya Mercedes-Benz ya kisasa wakati huo, iliyomfanya kujiunga na Orchestra Safari Sound (OSS), mwanzoni mwa miaka ya 1980, na akaleta mtindo wa Masantula Ngoma ya Mpwita, uliovuma kweli kweli na kukonga nyoyo ya mashabiki, akitunga na kuimba nyimbo kama 'Ni kweli', 'Mtoto wa Mjini', 'Haruna Kaka', 'Mwaka wa Watoto' na nyinginezo. King Kiki akawa mwamuziki wa kwanza Tanzania kumiliki aina hiyo ya gari, rekodi ambayo hadi sasa sijui kama imevunjwa au la.

Hata hivyo, mkataba wake wa miaka miwili ulikwisha na hakuongezewa tena, badala yake mwanamuziki mwenzake aliyekuwa naye kwenye bendi ya Orchetra Fauvette, Ndala Kasheba, anaja kuiongoza bendi hiyo na kuanzisha mtindo mpya wa Dukuduku, badala ya ule wake wa mwanzo, Masantula.

King Kiki alirejea nyumbani, Maquis, ambayo kwa wakati huo sasa ilibadilishwa jina la kuitwa Maquis Original, ambapo alitunga nyimbo kadhaa, lakini kuna zingine aliziimba kwa istadi mkubwa kama 'Double Double', 'Malokelee', na 'Anjelu.'

**KING KIKI DOUBLE O**

Aliondoka tena Maquis na kuanzisha bendi yake aliyoiita Orchestra King Kiki Double O, mwanzoni mwa miaka ya katikati na mwishoni mwa miaka ya 1980, akipata msaada wa vyombo vya muziki kutoka kwa mfanyabiashara na mwanasiasa maarufu wakati huo Dk Alex Khalid.

Alianzisha mtindo uliopendwa sana wa Embalasasa, Embalastop, Embala-shika breki, akitunga nyimbo zilizowachengua mashabiki wengi kama vile, 'Kitoto Kaanza Tambaa', 'Malalamiko', 'Dodom Capital', 'Lamanda', 'Pilikapilika Mtaa wa Samora' na nyingine nyingi, baadaye alikuwa mmoja wa waasisi na bendi y Sambulumaa ingawa hakukaa sana

**KITAMBAA CHEUPE**

Miaka ya 1990 aliungana tena na Kasheba na kuunda bendi ya Zaita Musica moja ya wimbo maarufu ni 'Kesi ya Khanga', baadaye bendi hiyo ilibadilishwa jina la kuitwa Ya Capital 'Wazee Sugu' ambapo ilifanya safari nchini Uingereza ambako ndiko walikokwenda kurekodi wimbo maarufu wa 'Nzibola', mwanzoni mwa miaka ya 2000, ambao umetokea kupendwa mno na kizazi cha sasa wakiuita, 'Kitambaa Cheupe.' Buriani Maestro King Kiki.

**Tuma meseji 0716 350534**



# Dunia yagawanyika kibali cha kukamatwa Netanyahu

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

AFRIKA Kusini imepongeza uamuzi wa makahama ya kimataifa ya Uhalifu (ICC) wa kutoa hati ya kumkamata Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu , aliyekuwa Waziri wa Ulinzi, Yoav Gallant na Kiongozi wa Hamas Mohammed Deif.

Netanyahu na mwenzake Gallant walishutumiwa kwa uhalifu dhidi ya Ubinadamu na uhalifu wa kivita katika eneo la Ukanda wa Gaza kuanzia Oktoba 8, 2023 hadi Mei 20, mwaka huu.

Idara ya uhusiano wa kimataifa wa Afrika Kusini (Dirco) ilisema kutolewa kwa hati ya kuwakamata viongozi hao watatu ni jambo la busara kushughulikia unyanyasaji wa haki za binadamu unaofanyika Gaza.

"Afrika Kusini imesisitiza kuendelea kujitolea kwake kuheshimu sheria za kimataifa na kutaka mataifa ambayo ni wanachama kutekeleza majukumu yao kulingana na utaratibu uliowekwa na sheria za Roma," ilisema.

Hata hivyo Afrika Kusini ilishindwa kutekeleza hati ya kumkamata kiongozi wa Sudan Omar al- Bashir alipokuwa ziarani Afrika Kusini mwezi Juni 2015.

Mwaka jana ,iliioneka mvutano wa kumkamata au kutomkamata Rais wa Russia Vladimir Putin kama atahudhuria kongamano la Brics katika mji wa Johanesburg.

Hata hivyo, Rais Putin aliepuka kukamatwa baada ya kuamua kufuatilia kongamano hilo kupitia njia ya video.

Mapema mwaka huu, Serikali ya Uingereza ilikosoa uamuzi wa Afrika Kusini wa kuwasilisha kesi dhidi ya Israel katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki ya mauaji ya kimbari katika vita vya Gaza.

Hata hivyo, Rais wa Marekani Joe Biden, ameonekana kughadhabishwa na hatua hiyo.

Marekani si mwanachama lakini kunaonekana kuwa na mgawanyiko hata miongoni mwa wanachama.

Serikali ya Uingereza haijatoa tamko lolote. Hata hivyo mbunge mmoja wa chama tawala cha Leba Emily Thornberry, alisema nchi yake inawajibu wa kutekeleza amri ya mahakama hiyo ya ICC ikihitajika kufanya hivyo iwapo Netanyahu atathubutu kuingia Uingereza.

"Tuliweka saini kuridhia mkataba wa Roma unaotoa taratibu za utendaji kazi wa mahakama hiyo,kwa hivyo majukumu yetu kuhusu hilo yako wazi. Kwa kifupi, tunaunga mkono mahakama hiyo ya kimataifa ICC.Ni koti huru na kama imeamua Netanyahu ana kesi ya kujibu mbele yao, na tayari wametoa waranti kwamba akamatwe, basi hatuna budi kuzingatia hatua hiyo, alisema

Kwa upande wa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amelaani uamuzi wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita na Uhalifu (ICC) wa kutoa waranti ya kukamatwa kwake akisema ni chuki dhidi yake na aliyekuwa Waziri wa Ulinzi Yoav Gallant.

Alisema ICC inawashtumu kwa kutumia uongo' kwamba wanawalenga raia kwa makusudi wakati wanafanya kila wanaloweza kuepusha mauaji.

Majaji wa ICC walisema kulikuwa na sababu za kuridhisha na kuamini kuwa watatu hao wana kesi ya kujibu kwa uhalifu wa vita kati ya Israel na Hamas.

**BBC**



Mabaki ya kombora la Kimarekani la ATACMS lililorushwa na Ukraine na kudunguliwa na mifumo ya ulinzi ya Russia juzi. **PICHA: IMAGO**

# Putin asema kombora 'Oreshnik' halizuiliki

**MOSCOW,** RUSSIA

BAADA ya Russia kuishambulia Ukraine kwa kombora zito, mkondo wa vita umechukua sura mpya ambayo imeongeza wasiwasi duniani kote.

Jana Ukraine, imelalamika kushuhudia matumizi ya silaha kali na kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua ya haraka dhidi ya Russia.

Akilihutubia taifa lake kwa njia ya televisheni juzi jioni, Rais wa Russia, Vladimir Putin alitangaza jeshi lake limetumia aina mpya ya kombora la masafa ya kati, kushambulia kituo cha kijeshi cha Ukraine.

Kulingana na Rais Putin, kombora jipya lililotumiwa kuishambulia Ukraine linajulikana kama Oreshnik, rangi ya khaki.

"Wataalamu wetu wa makombora waliliita Oreshnik. Majaribio yalifanikiwa. Lengo la uzinduzi lilifikiwa. Moja ya majengo makubwa na maarufu zaidi ya kiviwanda tangu enzi za Umoja wa Kisovieti ambayo bado huzalisha makombora na silaha nyingine leo liliharibiwa kwenye eneo la Ukraine katika jiji la Dnepropetrovsk (Dnipro)." alisema Rais Putin.

Awali Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alieleza shambulio hilo la Russia lilitumia makombora ya masafa marefu yenye uwezo wa kuvuka bara, maarufu kama ICBM.

Ukraine haikutoa maelezo zaidi juu ya shabaha iliyolengwa na Russia wala kiwango cha uharibifu uliotokana na shambulizi hilo.

Katika hotuba yake Putin alidai hatua ya jeshi la Russia ilikuwa jibu kwa uamuzi wa Marekani na Uingereza kuiruhusu Ukraine kushambulia maeneo ya ndani ya Russia kwa kutumia makombora ambayo imezipatia.

Putin aliongeza kuwa Russia inayo haki ya kulipiza kisasi dhidi ya nchi ambazo silaha zao zitatumiwa na Ukraine kushambulia ardhi yake.

Aliongeza kuwa kilichoanza kama mzozo wa kivita wa kieneo, imepanuka na kuchukua sura pana ya kidunia.

"Wakiendelea na mzozo wa Ukraine unaochochewa na nchi za Magharibi, Marekani na washirika wake wa NATO walitangaza hapo awali kwamba wanatoa ruhusa ya kutumiwa makombora yao ya masafa marefu na yenye usahihi wa hali ya juu katika maeneo ya ndani ya Russia. Wataalam wanafahamu vyema, na upande wetu tunasisitiza mara kwa mara hili, kwamba haiwezekani kutumia silaha hizo bila ushiriki wa moja kwa moja wa wataalam wa kijeshi kutoka nchi zinazozalisha silaha hizo." Alisema Rais Putin

Katika joto hilo la mvutano linalozidi kupanda, Volodymyr Zelensky amewataka Waukraine kuendelea kuwa watulivu na kuepuka kusambaza hofu wakati Russia ikizidisha shinikizo la mashambulizi makali ya anga.

Aidha, alisema jeshi lake iliyadungua makombora mawili ya Storm Shadow yaliyotengenezwa nchini Uingereza, lakini haikutoa ushahidi wowote.

Katika mwendelezo huo wa uhasama, Marekani imeweka vikwazo dhidi ya Gazprombank, benki ya tatu kwa ukubwa nchini Russia.

Waziri wa Fedha wa Marekani Janet Yellen, alisema vikwazo hivi vinakusudia kudhoofisha juhudi za kijeshi za Russia kwa kuzuia uwezo wake wa kukwepa vikwazo vilivyopo na kununua vifaa vya kijeshi.

**DW**

# Maelekezo ya Samia hati za kimila yatekelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mbunge wa Kavuu, Geophrey Pinda, amekabidhi hati za hakimiliki za kimila 691 kwa wananchi wa vijiji vya Ntilili na Igalukiro, kata ya Kasansa, Mlele mkoani Katavi.

Hafla ya kukabidhi hati hizo ilifanyika Novemba 21, mwaka huu, katika Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Kasansa na kuhudhuriwa na wataalam wa ardhi kutoka ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Katavi.

Naibu Waziri Pinda alisema hatua ya kukabidhi hati hizo ni ishara ya kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kupima ardhi ya nchi nzima.

"Hizi zote ni juhudi za Mama Samia Suluhu Hassan, anataka nchi nzima hii ipimwe, watu wake wawe na hivi vibali vya ardhi yao" alisema Pinda.

Alisema vijiji vya Ntilili na Igalukiro vimenufaika na mpango wa matumizi bora ya ardhi kupitia ufadhili wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) iliyowezesha uandaaji wa hati za kimila 691.

"Kupita mradi huu, Ofisi ya Makamu wa Rais imetufadhili tupime vijiji vinavoambatana na Mradi wake hapa juu (Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Uhifadhi wa Banowai) kwa hiyo wanufaika ni Ntilili na Igalukiro ambapo tumayarisha hati 691 zote zipo hapa," alisema.

Naye Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Katavi, Chediel Mrutu, aliwataka wanakijiji hao kuhifadhi hati hizo sehemu salama kwani zikiharibika si rahisi kupata nakala mbadala.

"Hizi hati ukiweka kwenye eneo ambalo linavuja itaharibika na ikiharibika siyo rahisi kupata nakala yake, Zamani watu walikuwa wanafanya lamination, hii hairuhusiwi, tafuta kibegi cha zuri na salama iweke na itunze," alisema Kamishina Mrutu.

Naye Ofisa Mipangomiji Mkoa wa Katavi, Flavian Masore, kupitia taarifa yake ya mpango wa matumizi bora ya ardhi katika Halmashauri ya Mpimbwe, alisema mpango huo umewezesha utoaji elimu ya ardhi sambamba na kutenga maeneo muhimu kwa ajili ya matumizi ya bora ya ardhi pamoja na kuandaa hati za ardhi.

"Vijiji vimewezeshwa kutenga maeneo ya matumizi mbalimbali ya kilimo, makazi vyanzo vya maji hifadhi za misitu maeneo ya malisho pamoja na kutunga sheria ndogo ndogo za kusimamia maeneo yaliyopangwa," alisema.

Wananchi wa vijiji vilivyonufaika na hati hizo kupitia kwa wenzao Joyce Mataluma na Robert Kasale, walifurahishwa wamefurahishwa na zoezi zima la utoaji hati milki ambapo wameahidi kuzitunza vizuri.

Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi na Uandaaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila katika halmashauri ya Mpimbwe unaowezeshwa na Tume ya Taifa ya Matumizi bora ya Ardhi kwa ufadhili wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kupitia Mradi wa urejeshwaji endelevu wa Mazingira na uhifadhi wa banowai umewezesha kuandaliwa jumla hati miliki za kimila 691 ambapo kijiji cha Igalukiro zimeandaliwa hati 277 na Ntilili zimeandaliwa hati 414.

Aidha, vijiji hivyo kupitia mradi huo vimepatiwa daftari la usajili la kijiji, cheti cha ardhi cha kijiji, ripoti maalumu ya matumizi bora ya ardhi, ramani ya mipaka ya kila kijiji pamoja na mhuri wa moto kwa ajili ya kusaidia kijiji kutoa hati kwa watu wasio na hati.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Mizengo Pinda akizungumza na wananchi wa vijiji vya Ntilili na Igalukiro, baada ya kuwakabidhi hati miliki za kimila 691, katika ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Kasansa, Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, mkoani Katavi, juzi. **PICHA: WANMM**

## Kata Kinondoni zapatiwa elimu ya ujasiriamali

**Na Maulid Mmbaga**

WAJASIRIAMALI katika Kata 20 za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali ili kuendesha biashara zao kwa usahihi.

Mafunzo hayo ambayo yameratibiwa na halmashauri hiyo, Taasisi ya Inquire International na Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), yametolewa kwa siku mbili ili kuwezesha kundi hilo kuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto za kibiashara wanazokutana nao.

Ofisa Maendeleo katika Halmashauri ya Kinondoni, Zephania Owigo, alisema wameamua kuyatoa baada ya kubaini kwamba elimu sahihi ya namna ya usimamizi wa biashara ni tatizo kubwa kwa kundi hilo.

"Mafunzo haya yanatolewa ili wale ambao wamepatiwa mikopo na wanaotarajia kupata siku zijazo wanapoingia katika biashara waweze kukabiliana na changamoto watakazokutana nazo na kujua namna ya kuendesha biashara kwa njia ambayo ni sahihi kwa ajili ya maendeleo yao," alisema Owigo.

Mkuu wa Kitivo cha Usimamizi wa Biashara Chuo cha OUT, Prof. Joseph Magali, alisema wajasiriamali kuwa na mbinu za kibiashara zinazomtofautisha na mwenzake ni suala la muhimu katika kuwavutia wateja na kuifanya biashara yake kuendelea na kupata mafanikio.

Pia alishauri wajasiriamali hao kujihusisha na mafunzo mbalimbali ya kibiashara yatakayowasaidia kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ya biashara kwakuwa kumeingia mifumo ya kisasa inayotumika katika nyanja hiyo ikiwamo Akili Mnemba (AI).

"Jambo ambalo pia, linawasumbua wajasiriamali wengi ni kutokutoa huduma bora, wanawaona wateja kama wao ndio wenye shida," alisema.

Alisema kuna dhana inasema, 'mteja ni mfalme' hivyo ni muhimu kuwajali kwasababu wale ndio wanaowaweka mjini.

"Kuna wateja ambao ni muhimu, ukimpoteza inakuwa sio sawa na wao huwa wanaangalia, wakianza kukusema kuwa huna huduma nzuri kwako kwa mfanyabiashara sio nzuri na itaathiri biashara yako," alisema Prof. Magari.

Aliwasisitiza wafanyabiashara na wajasiriamali hao kuhakikisha wanasikiliza vizuri na kwa umakini mafunzo hayo na waweze kuyatumia katika utekelezaji wa biashara zao.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Inquire International, Emmanuel Rusibamayila, alisema mafunzo hayo yametolewa kwa wajasiriamali kutoka kata 20 za Kinondoni, ili kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuwainua wanawake, vijana na wenye ulemavu.

# Kampeni soma na mkarafuu kukuza uchumi wa wanafunzi

**Na Christina Haule, MOROGORO**

SERIKALI mkoani hapa inatarajia kuanzisha kampeni ya soma na mkarafuu kwa kugawa miche 10 kwa kila mwanafunzi anayemaliza darasa la saba.

Lengo ni kumsaidia kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo ya shule ikiwamo kuondokana na mikopo ya elimu ya juu (Boom).

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Dk. Mussa Ally, alisema hayo jana wakati akizungumza kuhusu mkoa huo na mkakati wa kuendeleza mazao ya viungo kwa ajili ya maendeleo ya jamii na nchi nzima kwa ujumla.

Dk. Musa alisema kampeni ya soma na Mkarafuu itamsaidia kila mwanafunzi anayemaliza darasa la saba mkoani hapa kuwa na shamba katika eneo la wazazi wake lenye uwezo wa kumwingizia fedha baada ya miaka minne hadi mitano ya kupandwa.

Alisema kampeni hiyo itamsaidia pia mwanafunzi hata asipochaguliwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu, atapata fedha za mtaji wa kufanya biashara yoyote ikiwamo kununua bajaji, pikipiki (bodaboda) na hata kujenga nyumba na kuendesha maisha yake.

Mmoja wa wazazi, Rebecca William, aliishukuru serikali kwa somo hilo kwa sababu lina nafasi kubwa ya kumwingiza mtoto kwenye ajira mapema tofauti na wanafunzi wanaomaliza shule kwa sasa.

Alisema wanafunzi waliomaliza kabla ya soma na mkarafuu watakuwa wamekosa fursa kubwa ambayo ingewafaa katika maisha hasa katika kipindi cha changamoto za ajira nchini.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-40

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Tulichokuja kubaini ni kwamba tayari Materu na wapambe wake walikuwa wameshapita kwenye vyombo vingi vya habari na kujaribu kuzuia habari yoyote itakayomhusu.

Alifanikiwa kwa kiasi fulani, lakini baadhi ya waandishi za uchunguzi walipata fununu ya hilo wakatutafuta kuisaka habari hiyo.

Waandishi watatu wa magazeti walikutana sisi eneo la siri ambalo hata wao hawakujua ni wapi, wakamhoji Kamal kuhusu kuhusika kwake kwa mauaji ya mpenzi wake, ndipo alipowahadhithia kila kitu ikiwemo ushahidi unaoonyesha kuwa bosi yake, Materu ndiye aliyehusika kwa mauaji hayo.

Akawapa ushahidi wa maandishi na video ili hata kama akishtaki, basi ajikaange mwenyewe kwenye mafuta yake.

Siku tatu baadaye, kwa msaada wa kama dokta Shija, waandishi wengine wa habari za mitandao ya kijamii walipelekwa eneo lingine kwa ajili ya mahojiano.

Nao waliambiwa kila kitu, na kupewa ushahidi, ambao wanahabari zote walikuwa wakipewa kopi, hata flashi nazo zikipopiwa na kupestiwa, ili mwenyewe abaki na ushahidi halisi ambao ungeweza kumsaidia kuepuka kesi inayomkabili.

Baada ya kukamilisha zoezi hilo, ndipo habari zikaanza kurushwa, kitu ambacho kikabadilisha kila kitu. Kilibadilisha mtazamo wa raia na askari polisi juu ya mauaji ya mrembo Mariamu. Materu alikamatwa na kuletwa hapa. nadhani kwangu huu ndiyo mwisho wa ushahidi, vielelezo vyote tumevikabidhi, tunaachia mahakama tukufu," alimaliza afande Willy kutoa ushahidi wake ambao ulikuwa ni wa mwisho upande wa mashtaka. Kilichobaki sasa ilikuwa ni kupangwa tarehe kwa ajili ya siku ya washtakiwa kujitetea.

****************************************

Hakukuwa na pa kutemea mate mahakamani siku hiyo. Barabara za kueleka Mahakama Kuu zilifungwa. Ilikuwa ni siku ya hukumu ya kesi ya mauaji ya marehemu Mariamu. Hukumu hiyo ilisomwa mwaka mmoja baada ya mauaji.

Kila kitu kilikuwa tayari. Waandishi wa habari walikuwa wamejazana. Vyombo vingi vilikuwa laivu kutoka eneo la tukio. Ilikuwa ni kesi iliyogusa moja kwa moja jamii.

Jaji Ken Mahundi, akiongoza jopo wa wenzake wawili wanaounda jopo la majaji watatu. Alianza kwa kushukuru jinsi wananchi walivyokuwa wavumilivu kwa kipindi chote ambacho upelelezi uliokuwa umefanyika mpaka kasi hiyo imeletwa mahakamani pamoja na ushahidi hadi siku hiyo.




**"Shija ametuhakikisha kuwa yeye aliambiwa na mmoja na madaktari ambaye alitoa ushahidi kwa siri kuwa alipewa pesa na kupika ripoti. Ripoti ya pili iliyofanya na madaktari walioongozwa na dokta Shija ndiyo sahihi. Sasa ni kweli kuwa mpenzi wake alihusika na mauaji hayo kama baadaye Jeshi la Polisi lilivyoeleza? Si kweli. Baada ya ripoti sahihi, Materu na kundi lake waliona ni hatari kwao, walichotaka kujiondoa kwenye hatari, hivyo kumtengenezea kesi kijana Kamal. Kwanza yeye ndiye aliyetakiwa kuwa mlengwa wa kwanza kuuawa, lakini baadaye kibao kikageuka kwa Mariamu.**

Akaanza kwa kusema kumtaja marehemu Mariamu ambaye alifariki siku hiyo na alipopelekwa kufanyia uchunguzi ilibainisha kuwa alikuwa ameanguka kwenye mtaro ulio kando ya barabara ya Tabata.

Ikabainika kuwa alikuwa na ugonjwa na moyo, hivyo wakati anakimbia jogging, ugonjwa huo ulimpata ghafla na kuanguka.

Jaji akasema wananchi na ndugu hawakukubaliana na ripoti hilo, hivyo ikafanyika ya pili ambayo ilibaini kuwa aliuawa, kwani alikuwa amepigwa na kitu kizito kichogoni. Na ripoti hiyo ya pili ikakubalika na wote.

Jaji akasema kwa ushahidi uliopatikana mahamani ni kwamba ripoti ya kwanza ilipikwa kwa makusudi, na aliyefanya kazi hiyo ni mshtakiwa namba moja Boniphace Materu, kwani hakutaka ukweli ujulikane.

"Materu alitumia umaarufu na utajiri wake kupenyeza pesa kwa baadhi ya madaktari wakubwa ambao walizipitisha hadi kwa waliofanya uchunguzi na kupika ripoti hiyo. Ile presha ya wananchi na ndugu ndiyo iliyowabadilisha. Unashangaa kwa nini hospitali moja ifanye uchunguzi na mtu mmoja mara mbili na watoke na majibu mawili tofauti. Hapa ina maana moja si sahihi. Na ushahidi unaonyesha kuwa ule wa kwanza haukuwa sahihi, ushahidi upo hapa kutoka kwa baadhi ya madaktari akiwemo shahidi wetu Shija.

"Shija ametuhakikisha kuwa yeye aliambiwa na mmoja na madaktari ambaye alitoa ushahidi kwa siri kuwa alipewa pesa na kupika ripoti. Ripoti ya pili iliyofanya na madaktari walioongozwa na dokta Shija ndiyo sahihi. Sasa ni kweli kuwa mpenzi wake alihusika na mauaji hayo kama baadaye Jeshi la Polisi lilivyoeleza? Si kweli. Baada ya ripoti sahihi, Materu na kundi lake waliona ni hatari kwao, walichotaka kujiondoa kwenye hatari, hivyo kumtengenezea kesi kijana Kamal. Kwanza yeye ndiye aliyetakiwa kuwa mlengwa wa kwanza kuuawa, lakini baadaye kibao kikageuka kwa Mariamu.

Ushahidi uliosemwa hapa mahakami, unaonyesha Materu alituma watu waende nyumbani kwa Mariamu, na alipofika walimvizia kipindi atatoka nyumbani kwake saa moja usiku, moja akampiga na kitu kizito kichwani, wakambeba na kumpandisha kwenye gari. Huko wakamvua nguo alizovaa na kumvisha za mazoezi. Lengo lilikuwa ni kuonyesha kuwa alianguka alfajiri wakati akifanya mazoezi. Na hilo lilitimia kwani kesho yake alitekeleza hilo kwa kumtupa mtaroni. Madaktari wakapewa rushwa waidhinishe hilo.

Hapa inaonekana kabisa kuwa Kamal si muuaji wa mpenzi wake Mariamu. Kamal asingweza kumuua mpenzi wake ambao wamependana sana. Walitarajia kuoana. Nilisema hivyo nina maana kwani hata mauaji haya kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na penzi lao kuwa lenye uaminifu mkubwa." Jaji alizidi kutiririka.

Wakati Jaji akiongea, kila mmoja alikuwa makini kumsikiliza na kisa hicho kilionekana kuwateka sana watu kiasi kwamba hakuna hata aliyekohoa.

"Ushahidi wa meseji, simu za mkononi na klipu mbalimbali zilizokuwa kwenye flashi, zinaonyesha kuwa Materu alikuwa akimpenda sana Mariamu. Msichana huyo mrembo alikuwa na mchumba wa mfanyakazi wake Kamal. Materu alimpa ubosi wa kusimamia gereji kwa makusudi, ili kumuweka karibu na kumpata Mariamu. Alitongoza sana Mariamu, lakini msichana alikataa katakata. Alimuahidi zawadi mbalimbali, ikiwemo kumnunulia gari la kifahari na kumuahidi kumfungulia miradi mbalimbali, lakini alikataa.

Kilichofanyika baada ya hapo, ni kwamba Materu alimtisha Kamal kwa kutumia namba mbalimbali ambazo si za kwake, akitakiwa kumuacha mwanamke huyo la sivyo angeuawa.

Baada ya Kamal kumuambia mpenzi wake, Mariamu alikuwa muungawa, hakumwambia ni nani aliyefanya hivyo ingawa alimjua. Akapoza tu mpenzi wake, lakini akamwambia asiwe na wasiwasi hakuna wa kumuua.

Mariamu alichofanya ni kwenda kumwambia laivu Materu kuwa asidhani kumuua Kamal ndiye itakuwa tiketi ya kumpata. Badala yake akamthibitishia kuwa siku akisikia Kamal ameuawa na yeye atajoua, sasa sijui atakuwa amepata faida gani, kwa sababu hatompata. Ingawa hakusema kitu, lakini hili lilimkera Materu na moyoni akaahidi kumuonyesha. Na alichoamua ni kumuua tu, ili roho yake isiendelee kusononeka kumkosa Mariamu, msichana mrembo alikuwa mikononi kwa mfanyakazi wake, Kamal.

***Itaendelea Jumamosi***

# Tekeleza yaisimamisha Malindi Ligi Kuu Zanzibar

**Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TEKELEZA imefanikiwa kuondoka na pointi moja baada ya kulazimisha sare ya bao 1-1 na Malindi SC katika mechi ya mzunguko wa 12 ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi jioni.

Matokeo hayo yameifanya Malindi SC kufikisha pointi 23 na kusogea hadi nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar sawa na vinara wa ligi hiyo Mafunzo SC. Mwembe Makumbi City yenye pointi 23 yenyewe iko katika nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo wakati Tekeleza iko nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na pointi tatu baada ya kufungwa michezo tisa na kutoka sare mechi tatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Malindi, Omar Khamis Juma, alisema bado ina nafasi ya kurekebisha makosa yao na kubakia katika Ligi Kuu Zanzibar licha ya mwenendo mbaya wa matokeo wanayopata sasa.

Juma alisema kwa sasa timu yake inacheza kwa kiwango kizuri lakini anachohitaji zaidi safu ya ushambuliaji kufanya vyema ili kupata mabao.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wanafanikiwa kutengeneza nafasi nyingi za wazi lakini wanakosa umakini katika umaliziaji.

"Tunaendelea kurekebisha makosa ambayo tumeyabaini, tatizo kubwa kwa sasa ni washambuliaji wetu wanashindwa kutumia vizuri nafasi za kufunga, hawana utulivu, lakini nasisitiza bado muda upo wa kusahihisha makosa na kurejea katika ushindani," alisema kocha huyo.

Aliongeza katika michezo mitano waliyocheza mfululizo timu yake imebadilika kiuchezaji ikilinganishwa na walivyokuwa wakati msimu unaanza.

"Timu kwa inacheza vizuri katika nafasi ya kati, lakini pia wanafanikiwa kutengeneza nafasi ya kupenya kwa wapinzani, lakini bado maarifa na mbinu ya kufunga ndio yanawasumbua, tunaendelea kujiimarisha ili kupata ushindi.

Lakini napendwa kuwapongeza wachezaji wangu kwa kuendelea kucheza kwa matumaini katika michezo yote wanayoshuka uwanjani licha ya kutokuwa na matokeo mazuri, tunaamini tutapambana kuhakikisha michezo mitatu iliyobakia katika mzunguko wa kwanza tuvune pointi zote," aliongeza kocha huyo.

# TAOUSSI, ZAHERA WAIPONGEZA STARS KUFUZU AFCON 2025

**Na Adam Fungamwango**

SALAMU za pongezi kwa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kufuatia kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), zimeendelea kumiminika, baada ya Kocha Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, na Mwinyi Zahera, ambaye ni Mkurugenzi wa Ufundi wa Klabu ya Namungo, kusema wamefurahishwa na hatua hiyo.

Taoussi, amesema katika fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini kwao Morocco, atakuwa akishabikia taifa lake na Tanzania pia.

„Nina furaha sana kwa Tanzania kufuzu fainali za AFCON kwa sababu nawapenda watu wa hapa, nimekuwa hapa kwa zaidi ya miezi mwili sasa, naishi na watu vizuri, ni ishara njema kwangu hii ni kama nchi yangu ya pili.

Nawapongeza wachezaji, makocha na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), nimefurahi pia kwa sababu nina wachezaji kadhaa katika kikosi hicho, kwenye fainali hizo nitakuwa nikiisapoti timu yangu ya Morocco na Tanzania," alisema kocha huyo aliyeichukua Azam baada ya kuondoka kwa Youssouph Dabo.

Naye Zahera, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alisema alifahamu Taifa Stars ingefuzu, akiitaka sasa kufanya maandalizi ya fainali hizo.

„Watu wengi walikuwa wanatulaumu kabla ya mechi mbili za Stars kuwa sisi Wakongomani tumewafunga Watanzania wakati tayari tumeshapita, mimi binafsi sikuwa na wasiwasi kufuzu wa Stars, nilijua tu itakwenda kwenye fainali za Morocco na imekuwa hivyo, hayo yameshapita wasiangalie nyuma, inabidi sasa wajiandae, wafanya maandalizi kabambe ili kufanya vyema kwenye fainali hizo," alisema Zahera, kocha wa zamani wa Yanga na Polisi Tanzania.

Jumanne iliyopita, Stars ilitinga fainali ya AFCON kwa kuifunga Guinea bao 1-0 lililowekwa wavuni na Simon Msuva, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikimaliza na pointi 10, kwenye nafasi ya pili nyuma ya DR Congo, ikiwa ni fainali zake za nne tangu mwaka 1980.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (wa pili kushoto), akizungumza wakati wa uzinduzi wa 'Lite Your Imagination', jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Obinna Anyalebechi (kushoto), Msanii wa Bongofleva, Abdul Nasib 'Diamond Platnumz' (wa pili kulia) na Kedmon Mapana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ladies First kufanyika leo

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya sita ya riadha ya wanawake (Ladies first), yanatarajiwa kufanyika leo na kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha, alisema jijini jana mashindano hayo yatashirikisha wanariadha 155 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Msitha alisema mashindano yataambatana na semina ambayo itahusu masuala ya wanawake pamoja na mafunzo kwa upande wa makocha.

"Siku hiyo hiyo ya mashindano kutakuwa na semina fupi kwa wanawake, kutakuwa pia na mafunzo kwa makocha, mazoezi ya viungo," alisema Msitha.

Alisema washiriki watashindana kuanzia mbio za mita 50 hadi 10,000 kwa kupokezana vijiti na kurusha mkuki.

"Mashindano haya yatashirikisha wasichana wenye umri chini ya miaka 20 na lengo lake ni kuibua vipaji vya mchezo huo kwa wanawake," Msitha aliongeza.

Aliwataka Watanzania wajitokeze kwa wingi kushuhudia vipaji vya wanariadha hao chipukizi na hakuna kiingilio. Aliongeza pia kutakuwa na washiriki wa jogging zaidi ya 500 kutoka katika Wilaya ya Temeke.

## ZISIKUPITE

### WEST HAM YAMTAKA MCATEE

KLABU ya West Ham inatazamia kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City, James McAtee mwenye umri wa miaka 22, huku wakihofia kumpoteza fowadi wa Brazil, Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 27 Januari.***(Sun)***

### NISTELROOY ATAKA KUBAKI EPL

RUUD van Nistelrooy analenga kibarua kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kuondoka kwake Manchester United. ***(Mirror)***

### ASTON VILLA YAMTAKA LLORENTE

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery anataka kuimarisha safu yake ya ulinzi kwa kumsajili mlinzi wa kati wa Hispania, Diego Llorente mwenye umri wa miaka 31, kutoka Real Betis Januari, lakini mkataba wa muda mrefu wa beki huyo unaweza kuwa kikwazo. ***(Football Insider)***

### ....YAMUANIA PIA NA SANCET

ASTON Villa pia inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Oihan Sancet mwenye umri wa miaka 24, lakini hawana uhakika kama watatimiza masharti yake ya euro milioni 80. (£66.9m)***(Caught Offside)***

### ZIRKZEE AWINDWA JUVENTUS

JUVENTUS inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Manchester United na Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 23, huku mustakabali wa fowadi wao raia wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 24 ukiwa bado haujulikani. ***(CalcioMercato)***

### VICTOR OSIMHEN BEI JUU

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Victor Osimhen, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Galatasaray, atapatikana kwa euro milioni 75 msimu wa joto kwa mujibu wa kifungu cha kuachiliwa kilichowekwa na Klabu yake ya Napoli kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 na Napoli. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### N'CASTLE KUMPIGA BEI ISAK

KLABU ya Newcastle United inaweza kulenga kumuuza mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25 na kutumia fedha hizo kumnunua mbadala wake. ***(Football Insider)***

### TAH AGOMEA MKATABA MPYA

MLINZI wa kati wa Ujerumani, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 28, hatatia saini mkataba mpya na mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayer Leverkusen na anataka kuhamia Bayern Munich au Barcelona kwa uhamisho wa bila malipo. ***(Sky Sports)***

### SKRINIAR KUONDOKA PSG

BEKI wa Paris St-Germain, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kurejea Italia na kutua Juventus, Mslovakia huyo akiendelea kutatizika kupata muda wa kucheza katika klabu hiyo ya Ufaransa. ***(La Gazzetta dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ENDRICK HATOLEWI KWA MKOPO

●●●Klabu yake ya Real Madrid imeelezea hayo huku pia nyota huyo akisema....

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid haitarajiwi kumtoa kwa mkopo mshambuliaji Endrick, Januari, huku ripoti pia zikisema Mbrazil huyo hana nia ya kuondoka.

Endrick amekosa dakika za kucheza tangu ahamie Madrid majira ya kiangazi, huku mechi 10 za kinda huyo mwenye umri wa miaka 18 katika mashindano yote zikiwa zimefikisha dakika 122 tu za kucheza chini ya Kocha Carlo Ancelotti.

Hivi majuzi iliripotiwa Southampton imeonesha nia ya kumsajili Endrick kwa mkopo Januari wakitaka kujiondoa mkiani mwa ligi kuu ya England.

Lakini kwa mujibu wa Fabrizio Romano, nyota huyo hana mpango wa kwenda St Mary's.

Endrick ameridhika kuendelea kujifunza katika vipindi vya mazoezi huko Madrid, huku viongozi wa klabu pia wakiamini kuwa maendeleo yake yanatosha kubaki Santiago Bernabeu kwa muda.

Kilichotatiza mambo kwa Endrick ni uwepo wa mchezaji mwenzake aliyesajiliwa majira ya kiangazi, Kylian Mbappe, ambaye amepewa dakika muhimu licha ya matatizo ya mapema kushawishi timu.

Mfaransa huyo ana mabao nane katika mechi 16 lakini kuangalia zaidi ya takwimu kunazua maswali kuhusu kufaa kwake pamoja na Vinicius Junior katika wiki za mwanzo za msimu.

# James majanga tena Chelsea

**LONDON, England**

REECE James amepata jeraha lingine la msuli wa paja na atakosa safari ya Chelsea kumenyana na Leicester katika mchezo wa Ligi Kuu England wikendi hii, Kocha mkuu Enzo Maresca alisema katika mkutano na wanahabari jana.

James mwenye umri wa miaka 24, amekuwa na majeraha ya misuli ya mara kwa mara katika misimu michache iliyopita na alirejea tu baada ya kukaa nje kwa miezi mitano katika mechi ya Chelsea walipofungwa 2-1 na Liverpool Oktoba 20.

"Kwa hakika tuna mchezaji mmoja tu aliyejeruhiwa, huyo ni Reece. Kwa bahati mbaya, alihisi kitu kidogo na hatutaki kuchukua hatari yoyote kwa wikendi," alisema Maresca.

Alipoulizwa kuhusu hali halisi ya jeraha hilo, Maresca alisema, "Misuli. Ni tatizo la misuli. Hatutaki kuchukua hatari yoyote wikendi hii. Tunatumaini sio muda mrefu."

Nahodha huyo wa Chelsea alicheza kwa dakika 482 pekee kwenye kikosi cha kwanza msimu uliopita huku majeraha ya misuli ya paja yakimweka nje ya uwanja.

Alifanyiwa upasuaji Desemba 2023, kabla ya kupata jeraha lingine la msuli wa paja wakati wa ziara ya kujiandaa na msimu mpya wa klabu hiyo nchini Marekani msimu huu wa joto.

Maresca alisema Oktoba 18 kwamba alikuwa akitafuta kumrahisishia James kwenye picha ya kikosi cha kwanza polepole kwa kupunguza muda wake wa mechi kwani alihisi mwili wa mchezaji huyo hawezi kustahimili mechi mbili kwa wiki.

Tangu arejee, James alianza mechi mfululizo dhidi ya Liverpool, Newcastle, Manchester United na alicheza dakika nane za mwisho za sare ya Chelsea na Arsenal kabla ya mapumziko ya kimataifa.

# Lewandowski: Nilikaribia kutua Manchester United

**BARCELONA, Hispania**

ROBERT Lewandowski amekiri kwamba alitaka kujiunga na Manchester United, lakini Borussia Dortmund walizuia uhamisho wake kwenda Ligi Kuu England.

Mashetani Wekundu hao walijivunia kuwa na kikosi cha kuvutia mwaka wa 2012.

Wachezaji kama Nemanja Vidic, Ashley Young, Patrice Evra, Wayne Rooney na Rio Ferdinand walikuwa kwenye vitabu vya Old Trafford, wakiongoza klabu hiyo kutwaa taji la Ligi Kuu mwaka wa 2013.

Ingawa United hawakupungukiwa na vipaji vya kushambulia chini ya kocha mkuu Sir Alex Ferguson, walikaribia kumuongeza Lewandowski kwenye orodha ya kikosi chao.

Mshambuliaji huyo mashuhuri, ambaye alicheza Dortmund kati ya 2010 na 2014, sasa amefichua hadithi ya kweli nyuma ya kile ambacho kingekuwa msingi wa kuhamia Manchester.

"Nakumbuka mazungumzo na Sir Alex Ferguson," alisema Lewandowski akimwambia nyota wa zamani wa United Ferdinand katika kipindi chake cha Rio Ferdinand Presents.

"Niliamua kujiunga na Manchester United mwaka 2012.

"Nakumbuka mazungumzo yaliyokuwa kabla ya msimu mpya, tulikuwa tunacheza baadhi ya michezo. Nilijua kwamba yeye Ferguson angenipigia simu.

"Nilipata simu. Na wakati huo, unajua, Kiingereza changu, kilikuwa katika kiwango tofauti. Hasa ikiwa nitazungumza na mtu wa aina hii, Sir Alex Ferguson. Nilikuwa na wasiwasi sana na akapiga simu.

"Nilijua nilichopaswa kumwambia, Ndiyo, bila shaka, nataka kujiunga na Manchester United."

Wakati Lewandowski alikuwa amekubali kuachana na timu yake ya Ujerumani na kujiunga na wababe hao wa EPL, Dortmund hawakuwa tayari kumwachia nyota wao wa mabao aondoke.

"Nakumbuka pia mazungumzo na rais wa Dortmund," alisema mshambuliaji huyo wa sasa wa Barcelona.

"Aliniambia, wanamuhitaji. Hawataniuza kwa Manchester United kwa sababu mimi ni muhimu sana kwao. Haukuwa wakati muafaka.

"Lakini wakati ule nilisema ndio, hiyo ni kweli. Nilisema ndio nijiunge na Manchester United kwa sababu Sir Alex Ferguson akikupigia simu huwezi kusema hapana."



# GUARDIOLA ASAINI MIAKA MIWILI MAN CITY

**MANCHESTER, Englamd**

PEP Guardiola ametia saini mkataba mpya wa miaka miwili kuongeza muda wake kama kocha wa Manchester City, klabu hiyo imetangaza.

Guardiola mwenye umri wa miaka 53, alikubali mkataba utakaomweka Etihad hadi 2027.

Mkataba wake wa sasa ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Kuongezwa kwa muda kunamaanisha Guardiola atasherehekea miaka 10 akiwa City katika msimu wa majira ya joto wa 2026, baada ya kuwasili kutoka Bayern Munich mnamo 2016.

"Tangu mwanzo wa msimu, nimekuwa nikifikiria sana," alisema Guardiola.

"Nataka kuwa mkweli, nilifikiri huu msimu ungekuwa wa mwisho. Lakini matatizo tuliyokuwa nayo mwezi uliopita, nilihisi sasa haukuwa wakati muafaka kuondoka. Sikutaka kuiangusha klabu.

"Manchester City ina maana kubwa kwangu," aliongeza Guardiola.

"Tumepitia nyakati nyingi za kushangaza pamoja. Nina hisia maalum kwa klabu hii ya soka. Ndiyo maana nina furaha kusalia kwa misimu mingine miwili zaidi."

City, kulingana na vyanzo, walikuwa na wasiwasi Guardiola anaweza kujiuzulu mwishoni mwa msimu.

Uamuzi wake wa kusalia ni jambo kubwa, haswa kutokana na Mkurugenzi wa soka, Txiki Begiristain kuondoka katika klabu hiyo majira ya joto.

# WACHEZAJI KAGERA SUGAR WAAHIDI KUICHAPA AZAM

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wachezaji wa Kagera Sugar wameapa kuondoka na pointi tatu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Kocha Rachid Taoussi, amesema michezo miwili ya kirafiki waliocheza imesaidia kuwaweka vyema nyota wake ili kupambana kusaka ushindi leo.

Azam itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya kuwachapa mabingwa watetezi, Yanga bao 1-0, mechi iliyochezwa Novemba 2, mwaka huu.

Wenyeji Azam wako katika nafasi ya nne wakiwa na pointi 21 wakati Kagera Sugar itaingia uwanjani ikiwa kwenye nafasi ya 14 baada ya kujikusanyia pointi nane kibindoni.

Joseph Mahundi, mchezaji wa Kagera Sugar, amesema mapumziko ya Kalenda ya Kimataifa yamewafanya kupata muda mrefu wa kupumzika na kujiandaa kikamilifu kuelekea mchezo huo.

Mahundi alisema kwa sasa wachezaji wote wa timu hiyo wana morali na nguvu ya kurejea kwa kasi katika mikiki mikiki ya ligi hiyo, wakianza kuvuna pointi kutoka kwa Azam FC.

"Baada ya mapumziko ya kupisha michezo ya timu ya taifa, tulirejea kambini na tumefanya maandalizi ya kwenda kuikabili Azam, ni timu kubwa, lakini siku zote tukicheza na Azam panachimbika, mashabiki wataona kesho (leo), nini tutafanya," alisema Mahundi.

Naye Geofrey Manyasi, alikiri wanakwenda kucheza mchezo mgumu, lakini wao kama wachezaji wamejipanga kuhakikisha wanashinda kwa sababu wanataka kutoka chini walipo.

"Sisi kama wachezaji tumejipanga vizuri, tunajua Azam ni timu nzuri, mchezo utakuwa mgumu, lakini kwa jinsi tulivyojiandaa tuna imani tunashinda na kwa bahati nzuri siku hizi timu ikicheza vyema inashinda hata ugenini, hakuna shida yoyote ile," alisema Manyasi.

Taoussi, alisema baada ya Stars kutinga fainali za AFCON, wachezaji wake waliokuwa katika kikosi hicho wamerejea kwa furaha, na morali kubwa, hivyo anaamini itawasaidia pia kwenye mchezo wa leo.

"Tulifanya kazi na wachezaji waliobaki, mbali na wale waliokwenda kwenye michezo ya timu za taifa, tukacheza michezo miwili ya kirafiki ili kujiweka sawa, na hata wachezaji wetu waliokuwa Stars wamerejea, morali yao ingeongezeka kuelekea mchezo huu," alisema Taoussi.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana ya wanawake wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakifanya mazoezi kwenye Kituo cha TFF kilichoko Kigamboni, Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mechi zilizoko katika Kalenda ya Kimataifa. **PICHA: TFF**

# TFF: Taifa Stars iko salama

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kuwapo kwa sintofahamu ya huenda Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), itaondolewa kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limesema taarifa hizo si za kweli.

Taifa Stars imefuzu kushiriki AFCON 2025 baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi H ikiwa na pointi 10, nyuma ya vinara Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), yenye pointi 12.

TFF imesema inashangazwa na taarifa zinazosambaa mitandaoni kuhusu uhalali wa mchezaji, Mohammed Ame, ambaye alicheza mechi dhidi ya Guinea, ambayo ilimalizika kwa Stars kupata ushindi wa bao 1-0.

"Tunapenda kuufahamisha umma kuwa Ame ni miongoni mwa wachezaji 23waliokuwa wameorodheshwa kwa ajili ya mechi dhidi ya Guinea.Kabla ya mechi hiyo, wachezaji wa Stars walihaguliwa na timu pinzani pamoja na Kamishna ambapo waliruhusiwa kucheza," ilisema sehemu ya taarifa ya TFF.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema shirikisho hilo halijapokea taarifa yoyote Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuwa ushiriki wa Ame katika mechi hiyo haukuwa halali.

"Taarifa hizo za mitandaoni zisiwazuie Watanzania kuendelea kushangilia ushindi wa Taifa Stars," ilimaliza taarifa ya TFF.

Rais Samia Suluhu Hassan, aliipatia Stars Sh. milioni 700 kufuatia kukata tiketi ya kushiriki Fainali za AFCON zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

# Wasanii wapatiwe elimu ya uwekezaji

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa muziki nchini wamesema upo umuhimu wa wasanii kupatiwa elimu ya uwekezaji ili iwasaidie kutumia vyema vipato vyao vinavyotokana na kazi hiyo hasa pale shughuli hizo zinapofikia ukomo, imeelezwa.

Kauli hiyo iliyolewa jijini, Dar es Salaam jana katika hafla iliyowakutanisha wasanii kwa ajili ya kuwapatia elimu ya namna ya kutumia mifumo ya kidijitali kusambaza maudhui, iliyoandaliwa na Mdundo.Com.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Benki ya CRDB, Emmanuel Kiondo, alisema ipo mifano ya wasanii wengi ambao walifanikiwa kutengeneza fedha nyingi kupitia kazi hiyo lakini walirudi kuwa masikini baada ya kukumbwa na matatizo.

"Mtu badala ya kuwekeza fedha yake anayoipata kwa jasho, anaitumia vibaya katika mambo yasiyo ya msingi na akipata matatizo anapotea au wakati mwingine hata inaidi kumchangia. Kwa hiyo sisi kama CRDB, tunawapatia elimu ya namna ya kuwekeza kile wanachokipata, tunataka waache mambo ya kizamani,"alisema Kiondo.

Mdau mwingine wa muziki, Aman Martin, alisema kuna haja ya kuongeza uelewa kwa wasanii na wanaowasimamia ili wafahamu namna ya kutumia vizuri mifumo ya kidijitali katika kusambaza kazi zao.

Alisema bado kuna ugeni mwingi wa namna ya kutumia mifumo ya kidijitali katika kusambaza maudhui kwa wasanii wengi na kwamba kuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha wana kuwa na taarifa na maarifa ya kutosha ili iwasaidie kuepukana na shida ya kufanya kazi isiyo na manufaa.

"Tuachane na zile stori ambazo tumekuwa tukikutana nazo sana, mtu fulani alisaini mkataba ambao haukuwa na masilahi kwake, au mwingine hata hajui ni sehemu gani sahihi aiendee,"alisema Martin.

Aliongeza bila kujali ni maarufu au laa, msanii akitumia vizuri mifumo ya kidijitali kusambaza maudhui ya kazi yake, ni rahisi kunufaika.

"Cha msingi ni wanamuziki kufahamu namna mifumo hiyo ya kidijitali inavyoendeshwa na namna ya kuitumia katika kuinua au kutangaza kazi zao," Martin aliongeza.

Maureen Njeri, Mkurugenzi Mkazi wa Mdundo.Com, alisema wamerahisisha kazi kwa kuwaunganisha wasanii wa muziki kutoa maudhui yanayofaa na kuyasambaza kwenda kwa jamii kwa lengo la kuhakikisha kila mmoja wao ananufaika na kazi hiyo.

Michezo
Juma... Novemba 23, 2024
Nipashe

## Endrick hatolewi kwa mkopo

UKURASA 21





Kiungo wa Simba, Debora Fernandes (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Pamba Jiji FC, Daniel Joram, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza jana. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba yajiimarisha kileleni

## Yaifunga Pamba Jiji Kirumba, sasa yawageukia Waangola CAF...

**Na Faustine Feliciane**

BAO pekee la Leonel Ateba limeipa Simba pointi tatu muhimu mbele ya wenyeji Pamba Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza jana na kuendelea kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kufikisha pointi 28 baada ya kucheza michezo 11 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 24 ikicheza mechi moja pungufu huku Singida Black Stars wakishika nafasi ya tatu na pointi 23 kibindoni.

Mechi hiyo iliyokuwa na ushindani kuanzia dakika ya kwanza hadi filimbi ya mwisho ya mwamuzi, Hussein Katanga, ilipolia lakini ni Simba kutoka jijini, Dar es Salaam iliyoenda mapumziko wakiwa mbele na bao hilo lililofungwa kwa penalti na Ateba.

Mshambuliaji huyo kutoka Cameroon alifunga bao hilo na kufikisha goli la tatu msimu huu dakika ya 23 baada ya kuangushwa na beki wa Pamba Jiji ndani ya eneo la hatari na mwamuzi, Katanga kutoka mkoani, Tabora aliamuru pigo la penalti.

Simba walionekana kuutaka ushindi mapema baada ya kuanza kulishambulia lango la Pamba Jiji mapema mma ambapo dakika ya 17 ya mchezo krosi ya Ladack Chasambi ilimfikia, Chamou Karaboue, lakini shuti lake lilipaa juu.

Pamba Jiji ambao jana walicheza kwa kujituma walionekana kuzidiwa maarifa na wachezaji wa Simba kwa sababu licha ya kupanga mashambulizi hawakufanikiwa kuuvuka ukuta wa Wekundu wa Msimbazi ulioko chini ya Che Malone Fondouh.

Hadi dakika 45 za kipindi cha kwanza zinamalizika, Simba walikuwa mbele kwa bao hilo moja.

Kipindi cha pili kilianza kwa Simba kufanya mabadiliko baada ya Kocha, Fadlu Davids, kumtoa, Jean Charles Ahoua na nafasi yake kuchukuliwa na Kibu Denis huku pia akiwatoa Debora Fernandes Mavambo, Awesu Awesu na Chasambi na nafasi zao kuchukuliwa na Augustine Okojepha, Omary Omary na Abdulrazaq Hamza ambaye amerejea rasmi uwanjani baada ya kuwa nje zaidi ya mwezi mmoja akiuguza majeraha.

Hata hivyo mabadiliko hayo hayakubadili matokeo ya mchezo huo licha ya Simba kukosa mabao dakika ya 82 baada ya Kibu kupokea pasi ya Ateba lakini golikipa wa Pamba Jiji, Amos Yona alikuwa makini kwa kuutoa mpira nje na kuzalisha kona tasa.

Kabla ya shambulizi hilo, Pamba Jiji walikosa bao dakika ya 80 baada ya shuti la Samuel Antwi kudakwa kiufundi na kipa wa Simba, Moussa Camara.

Simba inarejea Dar es Salaam kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Marquis kutoka Angola itakayochezwa Novemba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa huku wawakilishi wengine wa Tanzania waliobakia kwenye michuano ya CAF, Yanga watashuka dimbani Jumanne kucheza mchezo wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Ligi Kuu Tanzania Bara itaendelea tena leo kwa Azam FC kuikaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Azam Complex wakati KenGold itawaalika Coastal Union na Mashujaa itacheza dhidi ya Namungo FC kwenye uwanja wake wa Lake Tanganyika ulioko mkoani, Kigoma.

## Yanga kuikaribisha Copco Kombe la FA

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Yanga wataanza kutetea taji hilo kwa kuwakaribisha Copco FC kutoka jijini, Mbeya katika hatua ya 64 bora wakati Simba itawavaa Kilimanjaro Wonderers, imefahamika.

Bingwa wa mashindano hayo hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Azam FC yenyewe imepangwa kucheza na Iringa FC wakati Coastal Union itakutana na Stand United huku Moro Kids itawafuata Pamba Jiji FC ya Mwanza na Namungo FC itawaalika Tanesco katika hatua hiyo.

Katika droo iliyofanyika jana Singida Black Stars yenyewe itacheza dhidi ya Magnet, KenGold itakutana na Mambali FC, Tukuyu Stars itawafuata Mashujaa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika huku KMC itajipanga kuwaalika Black Six na Tanzania Prisons itacheza dhidi ya Tandika United.

Mechi nyingine katika hatua hiyo itakuwa ni kati ya Tabora United dhidi ya Foysa Academy, Kagera Sugar itavaana na Rhino Rangers, Dodoma Jiji wao watapambana na Leo Tena huku Igunga United itasafiri kuwafuata Maafande wa JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Isamhuyo ulioko Mbweni, Dar es Salaam.

Ratiba hiyo inaonyesha Mbeya City watacheza dhidi ya Mapinduzi FC, Green Warriors watakutana na Hausung, Geita Gold wao watapimana ubavu na Ruvu Shooting, Bigman FC itawaalika Soccer City na Cosmopolitan itachuana na Nyota Academy.

Meneja Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto, alisema jana mechi za raundi ya tatu zitachezwa kati ya Desemba 6 na 8, mwaka huu.

"Tunazitakia maandalizi mazuri timu zote zilizofuzu hatua hii, tunaamini kila timu itajiandaa kufanya vizuri katika mashindano haya, tunatarajia ushindani utaongezeka kwa sababu hakuna timu itakayokuwa tayari kuondolewa kirahisi katika michuano hii," alisema Kizuguto.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >